BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,016,428,582/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#

UKURASA 3



## Wazazi watelekeza watoto watatu, baba aoa, mama aolewa




UKURASA 9

Nipashe
Jumapili Julai 24, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581016
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Nyongeza mishahara serikalini kizungumkuti

UKURASA 2



"Serikali inaweza kuangalia upya kibubu chake na kutumia taratibu zilizopo kubadilisha viwango hivi ambavyo si rafiki katu kwa wafanyakazi,"

**MWENYEKITI WA THTU, DK. PAUL LOISULIE**



"Ndugu zangu wafanyakazi, naomba tutulie, serikali itatoa ufafanuzi kuhusu nyongeza ya mishahara iliyotokea katika mishahara ya mwezi Julai, 2022."

**MSEMAJI WA SERIKALI, GERSON MSIGWA**



Malalamiko ya wafanyakazi tumeyaona, tutatoa tamko Dodoma Jumanne. Kuna kikao tulikuwa tumeandaa cha mambo ya kikokotoo (cha mafao).

**KATIBU MKUU WA TUCTA, HENRY MKUNDA**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama

UKURASA WA 3

### SERIKALI YAZUIA UINGIZAJI WA VIFARANGA VYA KUKU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema ifikapo Julai 30 mwaka huu, hakuna vifaranga vya kuku vitakavyoingizwa nchini na kwamba serikali haitoi tena,,,

UKURASA WA 4

### WANACHAMA 400 WATISHIA KURUDISHA KADI ZA CCM

ZAIDI ya wanachama 400 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Kata ya Mahina wilayani Nyamagana mkoani Mwanza wametishia kurudisha kadi...

UKURASA WA 11

### UNAMKATAA MUME WA KWANZA, UNARUDI NA TALAKA MRUDIANE

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya simulizi ya kijana Pazi na sakata la mkewe aliyemuacha na kuolewa na mwingine, japokuwa na huko hakudumu aliachika...

## ACT Wazalendo yaibuka na mambo sita mageuzi Polisi

UKURASA 2

## Migogoro ya ndoa chanzo ukatili nchini

UKURASA 8

**MICHEZO** SIMBA KUMENOGA, OUATTARA AFUNGUKA UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akiwa amemkamata dereva wa pikipiki maarufu bodaboda, baada ya kupita kwenye barabara ya mabasi ya mwendokasi, eneo la Kimara Baruti, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT Wazalendo yaibuka na hoja 6 mageuzi Polisi

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeibuka na mambo sita yakiwa ni msimamo na vipaumbele kwenye ajenda ya mageuzi ya Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama huku kikitaka Rais Samia Suluhu Hassan aungwe mkono katika hilo.

Vilevile, chama hicho kimesisitiza wananchi walifanya makosa kukubali kuingia katika mfumo wa vyama vingi pasina kufanya marekebisho stahiki ya kisheria, ikiwamo kuyabana majeshi katika kuingilia ustawi wa demokrasia nchini.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, katika hotuba yake aliyoitoa jana mjini Tanga katika Kongamano la Nne la Kitaifa la Tume Huru ya Uchaguzi Kuelekea Katiba Mpya, alisema hatua ya Rais ya kuunda tume ya kumshauri katika mageuzi hayo inapaswa kuungwa mkono.

"Tunaafiki hatua ya kuunda tume ya kumshauri Rais kuhusu mageuzi ya Jeshi la Polisi itayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, Rais anapaswa kuungwa mkono, kutiwa nguvu na kushauriwa ipasavyo kwenye ajenda ya mageuzi ya Jeshi la Polisi," alisema.

Duni alisema chama hicho kinaunga mkono hatua ambayo Rais Samia ameichukua kutaka mageuzi katika uendeshaji wa Jeshi la Polisi.

"Pili, mageuzi yanahitajika pia katika uendeshaji wa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vikosi vilivyoundwa kwa sababu maalum kama vile JKU na KMKM, wakati mwingine majeshi haya yanatumika kuwa vyombo vya kuumiza raia, hasa wakati wa uchaguzi.

"Ni vyema kwa vikosi hivi kujikita katika msingi wa kuanzishwa kwake badala ya kutumika kisiasa. Moja ya masuala ambayo marehemu Maalim Seif na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi walikubaliana kabla ya ACT-Wazalendo kushiriki kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni mageuzi katika uendeshaji wa vikosi vya SMZ," alikumbusha.

Alisema ni matumaini yao kuwa ukurasa ambao Rais Samia ameufungua wa mageuzi ya Jeshi la Polisi, utafunguliwa pia Zanzibar na Rais Mwinyi kwa kuvifanyia marekebisho makubwa vikosi vya SMZ.

Alilitaja jambo la tatu kuwa ni sheria zinazosimamia Jeshi la Polisi na vikosi vya ulinzi na usalama, zirekebishwe ili kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa demokrasia nchini.

"Kama tulivyobainisha kwenye Ilani ya Uchaguzi ya ACT-Wazalendo ya Mwaka 2020, tunahitaji marekebisho ya sheria kandamizi ya Jeshi la Polisi Tanzania na Huduma Saidizi Sura ya 322, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kifungu cha 43 (3), (4), na (6), ambayo pamoja na mambo mengine, inatoa mwanya wa wazi kwa polisi kuzuia uhuru wa kujumuika bila sababu yoyote ya msingi.

"Hivyo, kuna kukengeuka Katiba yetu ya nchi ya 1977 ibara ya 20 (1) inayoruhusu Uhuru wa Kukusanyika. Nne, tunahitaji mageuzi ya kifikra katika Jeshi la Polisi kutoka jeshi la kimabavu (police force) kwenda kwenye jeshi la kutoa huduma kwa raia (police service)," alishauri.

Duni alisema hayo yanahitaji mageuzi makubwa ya kikatiba, kisheria, kitaasisi na kifikra kuliondosha jeshi kutoka katika utamaduni wa kikoloni wa kutumia nguvu kubwa katika kutekeleza majukumu yake.

"Hivi sasa, Jeshi la Polisi limejijengea utamaduni sugu wa kutojali sheria kabisa. Licha ya sheria kuwataka polisi kuzingatia taratibu za kukamata, kupekua na kushika mali, kumekuwa hakuna mazingatio kabisa ya sheria.

"Ni jambo la kawaida kwa polisi kuvamia nyumba, kuvunja, kukamata, kupiga na kukamata mali bila hati ya kupekua na hati ya kukamata," alisisitiza.

Jambo la tano Duni alisema chama chao kinataka Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola viondokane na ushabiki wa kisiasa.

"Siyo kazi ya vyombo hivyo kama inavyoonekana sasa kuisaidia CCM kubaki madarakani. Ni jambo linalofadhaisha kuona kuwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vikipambana kuhakikisha vinaisaidia CCM ishinde," alidai.

Alisema ni wajibu wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuizuia CCM na chama kingine chochote kuvuruga uchaguzi.

Alisema Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama vinapaswa kuzingatia haki, usawa na weledi katika kutekeleza majukumu yake.

"Sita, mageuzi ya Jeshi la Polisi yaende sambamba na kasi ya dunia hasa kiteknolojia. ACT-Wazalendo tunahitaji Jeshi la kisasa linalowezeshwa kimafunzo, kirasilimali na kiteknolojia na uwezo kukabiliana na uhalifu wa ndani na wa kimataifa.

"Ninaomba niwakumbushe kuwa ni wajibu wetu kuonyesha njia. ACT-Wazalendo tutafanya uchambuzi wa kina wa sheria na kanuni zinazoongoza Jeshi la Polisi, vikosi vya SMZ na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuainisha mabadiliko ya kisheria yanayohitajika," aliahidi.

Alisema ni matumaini yao kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vyenye weledi na kuzingatia haki, vitakuwa ni manufaa kwa taifa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema kuwa ndani ya miaka 30 ya kuanzishwa kwa vyama vingi Tanzania, bado anaona kuna tatizo Jeshi la Polisi kutumika kisiasa kuumiza wananchi.

Shaibu alisema wananchi wamekuwa na hofu hasa nyakati za uchaguzi kutokana na mfumo mbovu unaotumiwa na serikali, akidai jeshi hilo linatumika kutokutenda haki kwa wagombea toka vyama vya upinzani.

"Ni miaka 30 sasa tangu kuanzishwa vyama vingi lakini hadi leo wagombea toka upinzani hawezi kutangazwa mpaka kutokee vurugu zinazosababishwa na jeshi hilo," alidai.

Shaibu alisema Katiba Mpya ndiyo mwarobaini utakaotokomeza shida hiyo.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Ismail Jussa, alisema serikali lazima itambue umuhimu wa Katiba Mpya na maslahi yake kwa Taifa.

Mwanzoni mwa wiki hii, Rais Samia alipomwapisha Mkuu mpya wa Jeshi la Polisi na Inspekta Jenerali (IJP) Camillus Wambura, aliweka wazi kuunda timu maalum ya wajumbe 12 itakayoangalia mwenendo wa vyombo vya ulinzi na usalama, akisisitiza kutakuwa na mabadiliko makubwa, wakianza na Jeshi la Polisi kisha vyombo vingine.

# Nyongeza mishahara serikalini kizungumkuti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NYONGEZA ya mishahara mipya kwa watumishi wa umma ambayo imelipwa juzi na serikali, imeibua malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi huku Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) likitarajiwa kutoa tamko keshokutwa jijini Dodoma.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza nyongeza ya mishahara kwa watumishi hao kwa asilimia 23.3.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Katibu wa TUCTA, Henry Mkunda, alisema mishahara mipya wameiona na baadhi ya wafanyakazi wanalalamika.

"Siku ya Jumanne (Julai 26, 2022) tutakuwa na nafasi nzuri ya kulitolea tamko suala hili. Malalamiko ya wafanyakazi tumeyaona, tutatoa tamko Dodoma. Kuna kikao tulikuwa tumeandaa cha mambo ya kikokotoo (cha mafao). Kwa hiyo, hili limetokea kama dharura na tutalijadili tukiwa Dodoma na kutoa tamko," aliahidi.

**KAULI YA THTU**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alisema wafanyakazi wengi wameona mshahara wa mwezi Julai wenye nyongeza lakini shida kubwa ya nyongeza hiyo iko kinyume kabisa cha matarajio yaliyokuwapo.

"Ongezeko ni dogo sana kwa walio wengi kiasi kwamba wanaona bora isingekuwapo kabisa. Imeibuka sintofahamu kubwa kwa wafanyakazi kutokana na ukweli kwamba ahadi ya nyongeza ya mshahara ilifanyika hadharani kiasi kwamba jamii yote inajua kwamba mambo ya wafanyakazi yatakuwa safi mwezi huu.

"Malalamiko pia ni mengi kutokana na ukweli kwamba nyongeza ya mshahara haiendani kabisa na gharama za maisha kwa sasa," Dk. Loisulie alibainisha.

Alisema hali hiyo itaongeza msongo wa mawazo kwa wafanyakazi, kuzidi kupungua kwa tija kazini, kuharibika uhusiano kati ya wafanyakazi na makundi mengine, hasa wanasiasa.

**NINI KIFANYIKE?**

Kiongozi huyo wa THTU alisema mwenye majibu sahihi ya nini kifanyike ni serikali na wameona mitandaoni kupitia kwa Msemaji Mkuu wa Serikali kwamba ufafanuzi utatolewa.

"Ni jambo jema na ni uungwana. Pamoja na kwamba tunasubiri ufafanuzi, sisi THTU tunapendekeza kwamba ukweli wa hali halisi uwekwe hadharani ili wafanyakazi wawe huru. Ukweli unaweza ukauma lakini utawaweka watu huru, busara ya heri lawama kuliko fedheha ituongoze katika hili.

"Kwa minajili ya kulinda uhusiano uliopo, serikali inaweza ikakaa na wafanyakazi kupitia viongozi wao ili kujadili kwa pamoja na kutoka na suluhisho linaloweza kurudisha faraja kwa wafanyakazi.

"Serikali inaweza kuangalia upya kibubu chake na kutumia taratibu zilizopo kubadilisha viwango hivi ambavyo si rafiki katu kwa wafanyakazi," alisema.

Dk. Loisulie alisema njia sahihi ya kurejesha faraja na matumaini kwa wafanyakazi ni kuboreshwa kwa viwango hivyo vya nyongeza.

**KAULI YA SERIKALI**

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, kupitia kurasa zake rasmi kwenye mitandao ya kijamii, ameligusia suala hilo, akisema: "Ndugu zangu wafanyakazi, naomba tutulie, serikali itatoa ufafanuzi kuhusu nyongeza ya mishahara iliyotokea katika mishahara ya mwezi Julai, 2022."

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (wa pili kushoto), akipokea kombe lililotolewa na Benki ya NMB Tawi la Nkinga, kwa Shule ya Sekondari Ziba, wilayani Igunga juzi, baada ya shule hiyo, kushika nafasi ya 10 kitaifa katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita mwaka huu. Mbunge huyo, alitoa zawadi ya 500,000/- kwa walimu wa shule hiyo na kuahidi kuwapa kompyuta 10. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba, mama watelekeza watoto na kuoa, kuolewa

**Na Idda Mushi,** ULANGA

MKUU wa Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, Ngolo Malenya, ameingilia kati tukio la kutelekezwa kwa mabinti watatu wanafunzi katika Kijiji cha Gombe wilayani humo.

Watoto hao wametelekezwa na wazazi wao walioachana na kila mmoja na kwenda kuoa na kuolewa na mwenzi mwingine huku maisha ya watoto hao yakiwa magumu na kukosa ulinzi na malezi stahili ya wazazi.

Ngolo ameingilia kati suala hilo, akizuru kijijini huko baada ya kupata taarifa za watoto hao wakati akifuatilia utekelezaji wa mkakati wa serikali wa kuwasaidia watoto wanaotoka kwenye kaya duni.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuagiza kutafutwa na kukamatwa kwa wazazi wote wawili wa watoto hao, baba mzazi, Thomas Ulanda na mama mzazi, Adelaida Nakashawa, ambao inadaiwa baba huyo sasa anaishi kijiji jirani na ameshaoa mwanamke mwingine.

Mkuu wa wilaya aliwasiliana na Mwenyekiti na Mwekezaji wa Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Graphite, John De Vries na kwenda naye ilipo familia hiyo kujionea hali iliyopo na kutoa mahitaji muhimu ya awali ya chakula, sukari, unga wa mahindi, mafuta ya kula na bidhaa nyingine na kuahidi kuwajengea nyumba katika eneo linalotafutwa na kijiji na kuwasomesha wototo hao.

"Nyumba ya sasa ni mbovu, kuna wakati watoto wanalazimika kukimbilia kwa majirani nyakati za mvua ili kujisitiri, lakini mtoto mkubwa wa kidato cha nne, ndiye anayetegemewa na wadogo zake wa darasa la saba mwenye umri wa miaka 13 na mdogo wa darasa la pili mwenye umri wa miaka tisa.

"Wakiwa na njaa au shida yoyote, hutembea umbali wa zaidi ya kilometa saba kumfuata dada yao hosteli au shuleni kuomba msaada, wanaishi kwa tabu sana," alisema Ngolo. Aliwashukuru majirani kwa muda wote kuwasaidia watoto hao kuendesha maisha yao na kufikia malengo yao, huku akimpongeza mfadhili aliyekubali kubeba majukumu yote muhimu kwa watoto hao. Binti mkubwa anayetegemewa na wenzake na mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Selina Kombani Ulanga (jina tunalihifadhi kutokana na umri wake) alipoulizwa na Nipashe kuhusu maisha yao, alisema mama yake aliwaacha akiwa darasa la sita mwaka 2017.

Alisema kuwa mama yao aliwaacha na baba yao na kurudi Julai 2018 lakini baadaye aliondoka tena miezi minne baadaye, yaani Novemba 2018. Baba yao pia aliondoka na kuwaacha baadaye.

"Nimekuwa ninafanya vibarua vya kulima siku za Jumamosi na mapumziko ili niweze kuwasaidia wadogo zangu wawili, nikienda shule huwa ninawaacha nyumbani peke yao na majirani huwasaidia chakula.

"Majirani wamekuwa msaada mkubwa sana kwetu, wazazi walianza kugombana na mama kuondoka na kutuacha na baba tu, na mama alikuwa akirudi mara moja moja kutuona," alisema.

Alibainisha kuwa awali walihamia kwenye nyumba ya mama yao wakiwa peke yao, lakini nyumba hiyo ilibomoka, wakarudi kwenye nyumba nyingine iliyokuwa ya baba na mama yao ambayo wameendelea kuishi hadi sasa ingawa ni chakavu na imebomoka.

"Mwaka 2020, baba alirudi kijijini hapa lakini akawa anaishi kwa mwanamke mwingine na mama hatujui aliko kwa sasa, ninasoma mbali ambako nimelazimika kupanga chumba kwa gharama ya shilingi elfu tano (Sh. 5,000) kwa mwezi ili kupunguza umbali wa kufika shuleni kila siku," alisema binti huyo.

Mmoja wa majirani na familia ya watoto hao, Hidaya Omary, alisema mara kadhaa alikuwa akiwasaidia watoto hao kwa kuwapatia chakula baada ya kuona wametelekezwa na ndiye aliyeibua tatizo la watoto hao baada ya kuwapo kwa mradi wa Msichana Wetu unaondeshwa na Shirika la Solidarmed wilayani Ulanga. Aliwaasa wazazi kutotelekeza watoto wao kutokana na ugumu wa maisha kwa kuwa huwafanya kuishi katika maisha magumu zaidi na wengine kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa ili kupata mahitaji muhimu.

Meneja wa Shirika la Solidarmed, Mary Yagala, alisema mradi huo ni wa majaribio ambapo katika Kijiji cha Gombe, waligundua kaya 15 zenye uhitaji na kwamba mradi huo unalenga kukata mnyororo wa umaskini kwenye kaya zenye watoto wa kike ambao wazazi wao huelimishwa na kuwezeshwa kiuchumi ili kutimiza ndoto za familia zao na kuwawezesha pia wasipate mimba katika umri mdogo.

# Serikali yazuia uingizaji vifaranga vya kuku nchini

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema ifikapo Julai 30 mwaka huu, hakuna vifaranga vya kuku vitakavyoingizwa nchini na kwamba serikali haitoi tena vibali vya kuingiza vifaranga hivyo.

Ulega alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati wa kikao cha wizara na wadau wa tasnia ya kuku kilicholenga kujadili namna ya kukuza tasnia hiyo na utekelezaji wa sheria ya mwaka 2006.

Serikali imekuwa ikizuia uingizaji wa vifaranga kutoka nje ya nchi ili kudhibiti ugonjwa wa mafua ya ndege kwa mifugo jamii ya ndege na kulinda wazalishaji wa kuku ndani ya nchi.

Akifungua mkutano huo uliojikita katika upatikanaji wa vifaranga vya kuku, chakula cha kuku na bei ya kuku sokoni, Ulega alisema ni mategemeo kuwa serikali haitaona vifaranga vinaingizwa nchini kutoka nje ya nchi.

Ulega alisema wanataka kuwapo kwa mfumo wa taarifa zinazohusu wazalishaji wa vifaranga vya kuku kuanzia wazalishaji wakubwa hadi wadogo ambao wamesajiliwa na kutoa taarifa serikalini ili kuiwezesha kujua kiwango cha uzalishaji na takwimu sahihi kuhusu mahitaji ya vifaranga nchini.

"Ni mategemeo yetu baada ya Julai 30 mwaka huu kutokuona mtu anaingiza vifaranga nchini kutoka mahali popote pale.

"Jambo la pili kuwapo na mfumo ambao utasaidia serikali kujua ni kiasi gani cha uzalishaji vifaranga ndani ya nchi yetu ili kujipima uwezo wetu na mahitaji yetu ndani ya nchi," alisema.

Awali Ulega alisema tasnia hiyo imekuwa kwa kasi miaka ya hivi karibuni kutokana na kuwaqpo kwa soko linalotokana na ongezeko la watu na kipato na ongezeko la uwekezaji na mazingira bora ya uwekezaji katika tasnia ya kuku.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Stephen Michael, alisema kutokana na umuhimu wa tasnia ya kuku katika Mpango Kabambe wa Sekta ya Mifugo wa Mwaka 2016, wamefanya tathmini na kubainisha kuwa hadi mwaka 2031, kutakuwa na upungufu wa nyama kwa tani milioni 1.8.

Kwa kuzingatia hali hiyo, alisema kuna haja kuchukua hatua, akisema tasnia hiyo ni rahisi na ikitiliwa mkazo, itasaidia katika kuongeza uzalishaji wa nyama nchini.

Michael ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema ufugaji wa kuku ni njia rahisi na ambayo haihitaji maeneo makubwa na miundombinu mingi tofauti na mifugo mingine. Alisema kikao hicho ni muhimu kwa kuwa kimeunganisha wadau wa tasnia hiyo pamoja na kutatua changamoto zilizopo kwa kuzingatia uwepo wa taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo kwa vijana na kinamama na vikundi mbalimbali ambao wengi wamejikita katika biashara ya kuku.

Katibu wa Chama cha Wadau wa Kuku Tanzania (PAT), Manase Mrindwa, alisema kero kubwa zinazowakabili ni chakula cha kuku kuwa kimefikia hadi Sh. 80,000 kwa mfuko mmoja na ongezeko hilo ni kutokana na bei ya mahindi na mashudu ya soya kwenye soko la Tanzania.

Kikao cha wadau wa tasnia ya kuku kilichoandaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kimejumuisha Menejimenti ya Wizara na Sekta ya Mifugo, wazalishaji wa vifaranga vya kuku, chakula cha kuku na wafugaji wa kuku ambao wametoa maoni mbalimbali ya namna ya kuboresha tasnia hiyo na kuomba kuwapo kwa vikao vya namna hiyo mara kwa mara ili kukuza tasnia hiyo kwa kuirasimisha na kuwapo kwa machinjio maalum kwa ajili ya kuku na bei elekezi ya kuku sokoni.


**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

**MAHALI: KIGOMA**

**MAOMBI NA. 9192 MWAKA 2022**

**ANTONY MHOMOLI: MWOMBAJI**

**DHIDI YA**
**MATHAYO WILSON: MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MATHAYO WILSON POPOTE ULIPO**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa **tarehe 11 Mwezi 08 Mwaka 2022 Saa 2.30 Asubuhi** mbele ya Mheshimiwa M. MWINYI Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu mimi na Lakiri / Muhuri wa Baraza hili leo **tarehe 19 Mwezi wa 07, Mwaka** 2022.

.................................
**MWENYEKITI**

**KUPOTEA KWA PASSPORT**



**BEATRICE DARABE BARAN** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 289273 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2020. Yeyote atakayeiona apige simu namba 0755548861 au atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye
**TAARIFA YA POLISI:**
**DAR/KIJ/RB/292011/2022**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA. 85 MWAKA 2022**

**SALAMA MATHIAS ANDREA: MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KIZA YASINI: MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: KIZA YASINI POPOTE ULIPO**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa **tarehe 15 Mwezi 08 Mwaka 2022 Saa 2.30 Asubuhi** mbele ya Mheshimiwa **M. MWINYI Mwenyekiti** wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu mimi na Lakiri / Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14 Mwezi wa 07, Mwaka 2022.

.................................
**MWENYEKITI**

# Wanachama 400 watishia kurudisha kadi za CCM

**Na Richard Makore,** MWANZA

ZAIDI ya wanachama 400 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Kata ya Mahina wilayani Nyamagana mkoani Mwanza wametishia kurudisha kadi zao za chama, wakishinikiza mashina 80 na matawi manane kufanya uchaguzi wa viongozi.

Akizungumza na Nipashe juzi katika kata hiyo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kata ya Mahina, Patric Bakari, alisema uchaguzi huo ngazi ya mashina na matawi umeshafanyika katika maeneo mengine, lakini wao wameshangaa kuona viongozi wamepatikana kwa kuteuliwa badala ya kuchaguliwa.

Alisema hajulikani nani aliteua viongozi hao kwa kuwa hata yeye kiongozi, hajawahi kuona wala kushiriki katika uchaguzi wa kuwapata.

Kiongozi huyo alisema kuwa kutokana na sakata hilo, wanachama wamekasirika na wametishia kurudisha kadi zao za chama kama haki haitatendwa.

Alisema kilichofanyika katika kata yake ni viongozi kutoa fomu moja kwa mgombea mmoja kwa kila nafasi na kuwanyima wengine nafasi ya kuchukua fomu kuomba kuchaguliwa, hivyo kuonekana kama wamepita bila kupingwa.

Alifafanua kuwa Katiba ya CCM inataka kila mtu apigiwe kura hata kama yupo peke yake, ipigwe kura ya ndiyo ama hapana, lakini kilichotokea wao wamepelekewa majina ya viongozi ambayo wanaamini kama yameteuliwa badala ya kufanya uchaguzi.

Alisema uchaguzi ngazi ya kata hiyo kwa ajili ya kuchagua mwenyekiti na viongozi wengine wa kata umepangwa kufanyika wiki ijayo, lakini itakuwa ngumu kutokana na kinachoendelea.

"Kata ya Mahina kuna rafu za ajabu kabisa, yaani mimi ni kiongozi ngazi ya kata, lakini sijui uchaguzi wa mshina na matawi ulifanyika lini, wapi na ulisimamiwa na nani," alisema Brakari.

Alisema wameandika barua wilayani kulalamika kuhusu suala hilo, lakini walikuwa hawajajibiwa chochote mpaka kufikia juzi.

Aliongeza kuwa kuna viongozi wa ngazi mbalimbali wanapanga safu za wanachama watakaowapigia kura na kwamba hiyo ndiyo sababu katika kata hiyo viongozi wake wa mashina na matawi wameteuliwa badala ya kuchaguliwa.

Akizungumza na Nipashe kuhusu sakata hilo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nyamagana, Zebedayo Athuman, alikiri kuwa na taarifa za mgogoro huo. Alisema eneo hilo lina mgogoro wa muda mrefu na alipoulizwa kuhusu wanachama kutaka kurudisha kadi za chama kutokana na kuteuliwa viongozi wasiowataka, Athuman alijibu kwa kifupi kuwa yeye hahusiki na suala hilo.

Alikiri kwamba wanachama wa mashina, matawi na Kata ya Mahina wilayani Nyamagana walifikisha suala hilo ngazi ya wilaya ingawa hakutaka kuweka wazi uamuzi uliochukuliwa na uongozi kutatua mgogoro huo.

# Vyuo vyapewa angalizo hasara wakati wa udahili

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema haitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu au taasisi itakayosababisha hasara au usumbufu kwa waombaji wa ngazi ya shahada ya awali wanaoomba hivi sasa kujiunga na mafunzo ya elimu ya juu.

Hivyo, imetoa wito kwa vyuo vyote vinavyodahili wanafunzi hao, kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa ili kuepuka usumbufu au hasara inayoweza kujitokeza kwa waombaji au kwa serikali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, alitoa angalizo hilo jana jijini Dar es Salaam kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja wakati akifunga maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Akizungumza katika maonyesho hayo, Michael alitaka hilo lizingatiwe ili kupunguza hasara kwa waombaji na kwa serikali kwa sababu hawatosita kuchukua hatua kwa mtu au taasisi iliyosababisha usumbufu, hasara, uzembe au ukiukwaji wa makusudi. Alisema taasisi za elimu ya juu zilizoshiriki maonyesho hayo, anaamini kila moja imejitathmini kwa haraka ni kwa kiasi gani wananchi na jamii kwa ujumla inafahamu na kutambua kazi inazofanya.

Pia alitoa wito kwa taasisi hizo kuendelea kujitangaza ndani na nje ya nchi ili watu wapate hamasa ya kujiunga katika vyuo hivyo itakayoongeza hadhi na fedha kupitia ongezeko la idadi ya wanafunzi watakaojiunga.

"Ninavipongeza vyuo vya nje vilivyoshiriki maonyesho haya. TCU mna wajibu wa kualika vyuo vingi vya nje ili vije kwenye maonyesho haya.

"Tunawapongeza wale wote waliowekeza katika vyuo, serikali itaendelea kuenzi ubia wa sekta binafsi na umma, tutaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi bila kuathiri ubora wa elimu itolewayo," alisema.

Dk. Michael alitoa wito kwa vyuo vya nje ya nchi kuja kuwekeza Tanzania kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan tayari ameifungua nchi katika uwekezaji.

Pia alisema maonyesho hayo yamezisaidia taasisi hizo kuongeza udahili wa wanafunzi, akitolea mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwamba awali walikuwa wamedahili wanafunzi 15,000 lakini hadi jana walifikia zaidi ya 30,000.

Katibu Mkuu huyo alitaja mafanikio yaliyopatikana kupitia ngazi ya vyuo vikuu katika serikali ya awamu ya sita ni pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti ubora ili kukidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa. Pia kuongeza idadi ya wanaojiunga na shahada ya kwanza, kutenga fedha za kuimarisha udhibiti ubora na uhuishaji wa mitaala na ufadhili unaofanywa na taasisi za fedha katika elimu.

Akiwa katika banda la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Dk. Michael alifurahishwa na ubunifu mbalimbali wa kisasa ambao unalenga kutatua matatizo ndani ya jamii.

"Chuo hiki kinafanya kazi nzuri na hii inaonyesha kuwa ni namna gani mmejipanga katika suala la ubunifu, ninawapongeza, zamani tulizoea kuona taasisi chache zinazofanya ubunifu lakini sasa chuo hiki kimepiga hatua kubwa," alipongeza.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema kupitia maonyesho hayo, wanaamini wanaendeleza uhusiano kati yao na vyuo vya elimu ya juu.

Mwakilishi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda, alisema wameridhishwa na maandalizi ya maonyesho hayo kwa sababu yameongeza idadi ya wanaodahiliwa na kuwezesha kuuza bidhaa mbalimbali.

Prof. Chibunda aliiomba serikali iendelee kuyaandaa maonyesho hayo na kuongeza idadi ya washiriki kutoka nchi za jirani ili waje kuona wanayoyafanya, akiahidi wataendelea kuyaboresha maonyesho hayo ili kuongeza tija kwa taasisi za elimu ya juu.




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael (kushoto), akionyeshwa mashine ya mfumo wa kupandisha maji kutoka kisimani kwa kutumia simu ya mkononi na mwanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere, Zacharia Lyimo, ikiwa ni ubunifu wake, wakati wa kufunga maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana

# RC Kafulila asisitiza weledi katika sensa

**Na Happy Severine, BARIADI**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amesema kutokana na umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi, kuna ulazima wa kuweka na kuwapata watu wenye elimu, sifa na maarifa watakaoiendesha kwa usahihi.

Ametoa angalizo kwa halmashauri zote mkoani humo kupitia wasimamizi na waangalizi wa sensa kutowaweka ndugu zao kwenye sensa na ikibainika, watachukuliwa hatua na kusisitiza kuwa wasiwapo watu watakaofanya kazi hiyo kutoka mikoa mingine kwa kuwa kila maeneo yana watu wake.

Kafulila alitoa maagizo hayo jana wakati wa kikao cha kamati ya sensa ngazi ya mkoa na kueleza kuwa jukumu hilo ni zito, nyeti na linahitaji kufanyika kwa umakini, hivyo waratibu 'wasilichukulie poa'. Alisema kumekuwa na tabia kwenye kazi kama hizo wahusika huwaweka ndugu zao, tena wanaotoka maeneo mengine, akionya kuwa ndani ya mkoa huo, hataki kuona suala hilo likifanyika na atakuwa makini kulifuatilia.

Aliongeza kuwa vyombo vya usalama na kamati ya mkoa inatakiwa kujua uzito wa jambo hilo na kuhakikisha linafanyika kwa uadilifu kwa kuzingatia sheria kwenye maeneo yao na linamalizika kama lilivyopangwa.

Mratibu wa Sensa Mkoa wa Simiyu, Susana Kulindwa, alisema maandalizi ya kazi hiyo yanaendelea kufanyika na mpaka jana, jumla ya watu 205 walikuwa wamepatiwa mafunzo na tayari usaili ngazi ya halmashauri kwa ajili ya nafasi za makarani na wasimamizi wa maudhui na Tehama umekamilika.

Baadhi ya wananchi wilayani hapa walisema kuwa wako tayari kuhesabiwa na wanaomba kazi hiyo ya kitaifa ifanyike kwa ufasaha ili kuwa na manufaa kwa wananchi wote.

## HABARI KITAIFA

# Wajawazito waonywa matumizi ya pombe

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MATUMIZI ya pombe kupindukia kwa kinamama wajawazito yanasababisha kujifungua mtoto mwenye tatizo la mdomo wazi, maarufu mdomo sungura.

Jijini Mwanza juzi, Dk. Baraka Maginga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanisa la Waadventist Wasabato, alitoa angalizo hilo alipozungumzia kambi maalum iliyowekwa hospitalini kwake kwa ajili ya kutibu watoto wenye midomo wazi pasina malipo yoyote.

Dk. Maginga aliitaka jamii kufuata maelekezo ya watalaamu ikiwamo ya kuzuia matumizi ya pombe kwa wajawazito na kutaka kuachana na imani potofu kwamba tatizo hilo linatokana na uchawi.

"Katika hospitali zetu tumekuwa tukipokea wastani wa watoto 100 wenye tatizo la mdomo wazi kwa mwaka. Hii inaonyesha kuwa tatizo hili limekua zaidi na kuwa tishio katika jamii.

"Hili tatizo halihusiani na mila zozote potofu, bali mara nyingi husababishwa na kurithishana kwa vinasaba pamoja na wanawake wajawazito kupuuzia masharti ya kitaalamu ikiwamo ya kuzuia matumizi ya vileo pamoja na kuacha kutumia dawa zinazotolewa kwa wajawazito wanapokwenda kliniki kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa," alisema.

Alibainisha kuwa hospitali hiyo inayomilikiwa na kanisa, imeanzisha kampeni maalum kwa ajili ya kutoa huduma ya upasuaji bila malipo kwa watoto na watu wenye midomo wazi.

"Tumeanza tayari kutoa huduma ya upasuaji na sasa tumehudumia watoto 19 na bado tunaendelea kupokea watoto wenye tatizo hilo ambapo mzazi anayeleta mtoto, atapatiwa sehemu ya kulala na mtoto atapata matibabu yote bure," alisema Dk. Maginga.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (aliyevaa kofia), akikata utepe kuzindua huduma ya Duka la Vodacom linalotembea, jijini Mwanza jana. Wengine ni Mkuu wa wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi (kushoto), Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa (wa pili kushoto) na kulia ni Mkuu wa Vodacom Tanzania Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aiangukia serikali uuzaji chakula nje ya nchi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MBUNGE wa Kishapu mkoani Shiyanga, Boniphace Butondo, ameiomba serikali kudhibiti uuzaji wa chakula nje ya nchi ili kuondoa mfumuko wa bei ya chakula nchini.

Butondo alitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Kishapu. Alisema bei ya vyakula sasa hivi inazidi kupanda kila kukicha kutokana na wafanyabiashara kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda kuja kununua vyakula nchini, hivyo kusababisha bei kuwa juu na kusababisha wananchi wa hali ya chini kushindwa kununua chakula. "Ninaiomba serikali kupitia Baraza hili la Madiwani idhibiti uuzaji wa vyakula nje ya nchi, hali inazidi kuwa mbaya, bei ya vyakula sasa hivi ipo juu sana. Tuchukue hatua ili kuwezesha wananchi wetu wanunue vyakula kwa bei ya chini na kuwapunguzia ukali wa maisha," alisema Butondo.

Aliwataka wananchi wilayani humo waache matumizi holela ya vyakula ikiwamo kupika pombe za kienyeji, bali wakitunze chakula ili kukabiliana na baa la njaa huko mbeleni kutokana na msimu wa mvua uliopita kutokuwa na mavuno mengi.

"Wananchi wa Kishapu wengi wao huwa wanalima mazao ya chakula kama mtama, uwele, viazi na mahindi, lakini msimu wa mvua uliopita hawakupata mavuno mengi, na wengine hawakuvuna kabisa kutokana na mazao kukauka na jua, hivyo kuna hatari ya kutokea baa la njaa," alitoa hadhari.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, pia aliwasisitiza wananchi wilayani humo wasiuze vyakula kiholela, bali wajiwekee akiba kwa kuwa mwaka huu kuna tishio kuwapo baa la njaa.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu, Emmanuel Johnson, kupitia idara ya kilimo, waanze kufanya tathmini kwa kila kijiji ili kujua kuna upungufu kiasi gani wa chakula kwa kila kaya na akiba iliyopo ya chakula.

Alisema tathmini hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kujua idadi kamili ya akiba ya chakula kilichopo na mahitaji kwa kila eneo, ili kukitokea baa la njaa, itakuwa virahisi kutoa msaada wa chakula kwa wananchi.

Aliwataka wataalamu na viongozi kuanzia ngazi ya vitongoji, watoe elimu ipasavyo kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza vyakula, hasa katika kipindi hiki ambapo dalili inaonyesha siyo nzuri sababu ya kuwapo kwa upungufu wa chakula.

# Ndalichako aona mapinduzi katika sekta ya mifugo nchini

**Na Ashton Balaigwa,** MVOMERO

SERIKALI imesema inakusudia kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo kwa kuongeza thamani ya mazao ya mifugo, ikiwamo nyama na ngozi, kupitia mradi wa machinjio ya kisasa ya Kiwanda cha Nguru Hills kilichoko wilayani Mvomero mkoani Morogoro.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo juzi alipotembelea mradi wa uendelezaji wa shamba la kunenepesha mifugo na machinjio ya kisasa wa Nguru Hills yaliyoko wilayani Mvomero.

Alisema mradi huo ambao unaendeshwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Kampuni ya Eclipse Investiment LLC na Kampuni ya Busara Investment LLP, ni wa aina yake kwa kuwa utaleta faida kubwa kwa wafugaji na Watanzania wengine.

Prof. Ndalichako alisema mbali na upatikanaji wa nyama wenye ubora, ngozi zitakazopatikana kutoka kwenye kiwanda hicho, pia zitakuwa na ubora wa hali ya juu.

"Pamoja na kwamba hivi sasa hiki kiwanda kiko kwenye majaribio, tayari fursa zimeanza kufunguliwa kwa wafugaji na vijana wakiwamo wa Wilaya ya Mvomero," alisema. Prof. Ndalichako.

"Tayari vipo vikundi vitatu vya vijana vimepata mkopo kutoka Halmashauri ya Mvomero, vitafanya kazi ya unenepeshaji mifugo kwa kuandaa mashamba kwa ajili ya malisho ya mifugo," alisema.

Waziri Ndalichako alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhamasisha uwekezaji wenye tija na kufungua fursa nje ya nchi kwa kuwa masoko ya kuuza nyama nje tayari yamepatikana ya kutosha.

Alisema bidhaa zitakazozalishwa kutoka kwenye kiwanda hicho mbali na kuuzwa kwenye soko la ndani, pia zitasafirishwa nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji PSSSF, Fortunatus Magambo, alisema mfuko huo kwenye mradi huo unamiliki asilimia 39 ya hisa, wawekezaji wenza Kampuni ya Eclipse Investiment LLC kutoka Oman wanamiliki asilimia 46 na Kampuni ya Busara Investment LLP ya nchini ina asilimia 15.

"Sisi kama PSSSF tumeweka Sh. bilioni 8.3 na tulikubaliana kwamba mradi lazima ukidhi mahitaji ya kimataifa," alisema Magambo.

Alisema machinjio ya kiwanda hicho yatakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 hadi 1,500 kwa siku.

"Kitakachofanyika Kampuni ya Nguru itatunua ng'ombe wenye umri usiozidi miaka minne na wenye uzito wa wastani wa kilo 25 hadi 300 na watatunzwa kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu ili kufikia uzito wa wastani wa kilo 500 na kupata historia ya mifugo husika kabla ya kuwachinja," alisema. Magambo alisema mradi una miundombinu inayohitajika ikiwamo eneo la malisho hekta 2,328 lenye uwezo wa kulisha ng'ombe 10,000 na mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja. Pia visima vitano vya maji vyenye uwezo wa kutoa lita 20,000 kwa saa na kujengwa barabara za kuingia kwenye ranchi ikiwa ni pamoja na mabwawa.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji PSSSF alitaja soko kuu la bidhaa za nyama ni katika nchi za Mashariki ya Kati.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash, alisema kuwapo kiwanda hicho kutawanufaisha wafugaji wengi kupata fursa ya kuleta mifugo yao kuiuza na kwa kiasi kikubwa kitapunguza migogoro inayojitokeza baina ya wakulima na wafugaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa serikali kuzuia uingizaji wa vifaranga toka nje ni mwafaka

**SERIKALI** jana kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ilitangaza kuwa kuanzia Julai 30, mwaka huu, hakuna vifaranga vya kuku vitakavyoingizwa nchini kutoka nje na hakutakuwa na kibali kitakachotolewa kwa ajili ya jambo hilo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hayo jana jijini Dodoma wakati wa kikao cha wizara na wadau wa tasnia ya kuku, huku akibainisha kwamba lengo la kuzuia uingizaji huo ni kuwalinda wazalishaji wa ndani. Sababu nyingine ni utekelezaji wa sheria inayosimamia tasnia hiyo pamoja na kudhibiti ugonjwa wa mafua ya ndege kwa mifugo jamii ya ndege.

Waziri Ulega alisema baada ya hapo, serikali inatarajia kuona uzalishaji wa vifaranga kutoka ndani ukishamiri na kwamba kwa zuio hilo la uingizaji wa mbegu hizo za kuku, serikali itapata mwanga kamili juu ya kiwango cha uzalishaji wa vifaranga nchini.

Hatua ambayo imechukuliwa na serikali ni mwafaka na inapaswa kuungwa mkono, kwanza, kwa kulinda wazalishaji wa ndani ikiwa ni njia mojawapo ya uwezeshaji wazawa na wawekezaji wa ndani kiuchumi na pili, kudhibiti mlipuko wa magonjwa kama mafua ya ndege ambayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu.

Pamoja na kuungwa mkono, ni jambo la kushangaza kwamba mpaka sasa, wakati nchi ikiwa na zaidi ya miaka 60 ya Uhuru, haijafikia kiwango cha kujitosheleza katika uzalishaji wa vifaranga kwa ajili ya kuendeleza tasnia ya kuku pamoja na kuwawezesha hata wafugaji wadogo kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

Tunasema hivyo kwa sababu kama taifa tunapaswa kujitegemea kwa baadhi ya mambo kwa kuwa nchi ina utajiri mwingi wa rasilimali zinazoweza kuiletea sifa ikiwamo ufugaji wa kuku, wote wa kisasa na wa kienyeji.

Jambo la kujiuliza, inakuwaje nchi inaagiza vifaranga ilhali kuna maofisa mifugo na maofisa ugani kuanzia ngazi ya halmashauri hadi wizara? Pia kuna taasisi nyingi zinazohamasisha ufugaji wa wanyama wakiwamo aina ya ndege lakini ni kwa nini ifike hatua ya kuagiza vifaranga hadi sasa?


Hayo ni baadhi ya mambo ambayo kila Mtanzania anajiuliza kwamba inakuwaje mpaka sasa vifaranga vinatoka nje ya nchi wakati kuna fursa ya kuzalisha kwa wingi na hatimaye wananchi kupata nyama ya kuku bila matatizo.

Pamoja na hayo, serikali itengeneze fursa na uwezeshaji kwa wafugaji wa kuku nchini kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa. Taasisi za kifedha kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inapaswa kuchukua zuio hilo kama fursa ya kuwawezesha wazalishaji wa vifaranga mikopo ya mashine za kutotoleshea ili kupata mbegu nyingi kwa ajili ya wafugaji.

Tanzania kwa sasa inatekeleza sera ya viwanda kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa taifa. Kwa mantiki hiyo, sekta ya mifugo ni moja ya maeneo yanayopewa kipaumbele, hivyo ni wakati mwafaka kuhakikisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kutotolesha vifaranga, vinaanzishwa kwa wingi ili kuziba pengo la vile vinavyotoka nje.

Kwa kufanya hivyo, nchi itakuwa na uwezo wa kuwa na vifaranga vya kutosha ambavyo vitaamsha ari na hamasa kwa ukuaji wa tasnia hiyo ikiwamo kuwawezesha wafugaji wadogo, wa kati na wakubwa kufuga kibiashara na hatimaye kukuza uchumi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vituo vya daladala vilivyoko barabara hizi vingepanuliwa

Na Sabato Kasika

**MIJI** mikubwa ikiwamo Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha na mingine nchini, inaendelea kukua kwa kasi siku hadi siku, ukuaji wake huo unajitofautisha ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita.

Jiji la Dar es Salaam ni moja ya mfano wa ukuaji wa miji hiyo, kwani, lina idadi kubwa ya watu na hata wingi wa magari yakiwamo ya usafiri wa umma ambayo ni maarufu kama daladala, kuliko mikoa mingine nchini.

Wingi huo wa daladala ni unafuu kwa wakazi wake, kwani unasaidia kuwafanya wapate usafiri na kuwahi katika shughuli zao za kila siku katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake.

Lakini pamoja na unafuu huo, kuna tatizo moja katika usafiri huo, ambalo ninadhani ni vyema mamlaka husika ikalitafutia ufumbuzi kabla halijasababisha madhara kwa abiria na hata waenda kwa miguu.

Tatizo lenyewe ni ufinyu au udogo wa vituo vya daladala, ambao wakati mwingine huchangia madereva wa daladala kuegesha magari barabarani kupakia au kushusha abiria, hali ambayo inaweza kusababisha ajali.

> **Tatizo lenyewe ni ufinyu au udogo wa vituo vya daladala, ambao wakati mwingine huchangia madereva wa daladala kuegesha magari barabarani kupakia au kushusha abiria, hali ambayo inaweza kusababisha ajali.**

Karibu maeneo mengi ya jiji, vituo vyake ni vidogo havina uwezo wa kuhudumia daladala zaidi ya tano kwa wakati mmoja, badala yake madereva wanapokuta vimejaa, hushusha na kupakia abiria pembeni.

Mfano mmojawapo ni kwenye Barabara ya Maendeleo na ile kuelekea Segerea hadi Kinyerezi kutokea Tabata Relini. Vituo vya daladala ni vidogo ambavyo ingefaa vipanuliwe ili kutowaweka abiria na waenda kwa miguu katika hatari ya kupata ajali.

Ninaamini kwamba kitendo cha daladala kuegeshwa barabarani kushusha au kupakia abiria, kinaweza kusababisha ajali hasa pale inapopsimama ghafla wakati kuna mgari mengine yakuja nyuma.

Mbali na ajali, wakati mwingine uegeshaji huo unaosababishwa na ufinyu wa vituo, unaweza kuchangia kuwapo kwa foleni za magari zisizo za lazima, hivyo ninadhani kuna umuhimu wa kuvipanua.

Lakini pia wapo baadhi ya madereva hupenda kupakilia abiria nje ya vituo hasa maeneo ya mwanzo na mwisho wa vituo, hali inayosababisha msongamano mkubwa wa magari mengine.

Msongamano huo wa magari mengine unaosababishwa na baadhi ya madereva hao, hutokana na daladala kuziba upande mmoja na kufanya watumiaji wengine wa bara barabara kushindwa kupita na hivyo kuwa kero.

Wakati vituo hivyo vikiwa ni vifinyu, baadhi ya wafanyabiashara wadogo nao wamevigeuza kuwa mahali pa kufanyia shughuli zao na kusababisha abiria kukosa sehemu ya kupumzika wanaposubiri usafiri.

Mazingira hayo yote na mengine katika vituo hivyo, ingefaa yaboreshwe, kwani mbali na Barabara ya Mandela, hali hiyo ipo maeneo mengi ya jiji hasa vituo kutokuwa na uwezo wa kutumiwa na daladala nyingi kwa wakati mmoja.

Wakati hali ikiwa hivyo, ruti mpya za daladala zimekuwa zikiendelea kuongezeka kutokana na jiji linavyopanuka, lakini kwenye ruti mpya barabara zake hazina vituo vinavyoeleweka, hasa pembezoni mwa jiji.

Iwapo ruti hizo zitaendelea bila kuwa na vituo vya daladala, maana yake ni kwamba madereva wa daladala wataendelea kushusha na kupakia abiria barabarani, mazingira ambayo kimsingi si salama.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hatimaye nimepata uwakili, je, nitakuwa kaka Lakha? – 2



Na Pascal Mayalla

KWA wasomaji wapya, hii ni hadithi ya safari yangu ya ndoto ya kuwa wakili, iliyoanzia Mwanza mwaka 1976 takriban miaka 45 iliyopita. Hatimaye nimekuwa wakili mwaka huu, hivyo kujiuliza, je, bado naweza kuwa kama Wakili Murtaza Lakha?

Wiki iliyopita, hadithi hii iliishia baba yangu Mzee Andrew Mayalla, aliyekuwa ofisa wa serikali Mwanza na familia nzima kuhamishwa usiku usiku kurejeshwa kijijini kisha huko akafuatwa na watu wa kazini kwake, akachukuliwa na kupelekwa kusikojulikana. Nikidhani amesafiri, nami nikafuatwa na baba yangu mdogo, Mzee Mathew Kasanga kuja kuishi nyumbani kwake Dar es Salaam bila kuambiwa nini kilimtokea Mzee Mayalla.

Niwarudishe nyuma kidogo, kumbe ile hama hama ya usiku kwa majirani wanne wa eneo la Isamilo ya Chini ya mwaka 1976 na majirani zetu wote, Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Ofisa Usalama wa Mkoa, Ofisa Usalama wa Wilaya na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambao tuliishi nyumba zilizofuatana, haikuishia kwetu tu.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Peter Kisumo, naye alistaafishwa, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Samweli Pundugu alistaafishwa, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Emelio Mzena alistaafishwa! Hawa ni maofisa wa kiutendaji serikalini.

Wanasiasa nao hawakubaki salama. Makamu wa Pili wa Rais, Rashidi Kawawa, aliondolewa; Waziri wa Mambo ya Ndani, Ali Hassan Mwinyi, aliambiwa kuandika barua ya kujiuzulu. Waziri wa Usalama wa Taifa, Peter Siyovelwa naye aliamuriwa kuandika barua.

Nikiwa darasa la 5, tayari nimeshaanza kusoma magazeti ya Mzalendo, siku za Jumapili, Kesi ya Mauaji Mwanza ilipoanza kurindima na kuripotiwa kwenye kipindi cha Majira cha Radio Tanzania (RTD) na Jumapili kwenye gazeti la Mzalendo, ikawa mara yangu ya kwanza kujua baba yangu, Mzee Mayalla, alikuwa ni nani, alikuwa anafanya kazi wapi baada ya kuona jina lake gazetini kuwa ni miongoni mwa washtakiwa kesi hiyo ya mauaji Mwanza.

Unapokuwa unadhani baba yako yuko safarini, unapokuja kujua kwa kusoma gazetini na si kuelezwa rasmi nyumbani, ulikuwa mshtuko wa aina yake. Kitendo tu cha kusikia mtu mwenye upendo wa aina ya Mzee Mayalla, hata kuua tu panya hawezi kusikia anahusika na kesi ya mauaji! Huwezi amini!.

Kitu cha kwanza, nilichanganyikiwa kwa nini sikuambiwa mpaka kuja kusikia redioni na kusoma gazetini. Nilipata unyanyapaa fulani. Nyumbani ulikuwa ukifanya kosa kubwa adhabu yako ni kupigwa na kuambiwa kulala njaa. Kwa vile mimi si mtoto wa kuzaliwa na Mama Kasanga, angalau adhabu za bakora ziliniepuka lakini kiukweli Mama K ni mkali, hataki ujinga ujinga. Kwa vile kulala njaa kwao ilikuwa adhabu, mimi nikaanzisha 'maradhi ya kutokula' na nikawa sili usiku.

Nilikuwa bonge lakini hii kesi ya baba ikaanza kunikondesha. Baada ya kujua baba ana kesi, nikajenga tabia na kujifunza kufanya uchunguzi kuhusu kesi za mauaji na kubaini kuwa kumbe hukumu yake ni kunyongwa mpaka kufa!. Nilitafakari itakuwaje baba akikutwa na hatia? Kiukweli iliniumiza sana akili.

Ninavyomfahamu Mzee Mayalla, kuambiwa huyu ni muuaji, unajua kabisa si kweli. Baba alikuwa anatetewa na Wakili Murtaza Lakha, nadhani kwa wakati huo alikuwa mmoja wa mawakili bora nchini. Nadhani baba alitetewa na Lakha kwa sababu wakati huo Mzee Mathew Kasanga tayari alikuwa tajiri mkubwa.

Enzi hizo magari ya mawaziri yalikuwa Peogeot 504, ndilo lililokuwa gari la Mzee Kasanga. Mama naye ana gari lake, Renault na kuna gari la kuhudumia familia Volkswagen Combi. Pia kuna gari la shamba, Landrover 109 Short Chasis ya kibanda wazi. Hapo Drive In, nyumbani kwetu ni moja ya nyumba chache kuwa na TV na video. Pamoja na kwamba palikuwa na maisha bora, nilikuwa nakonda kwa kuhofia hatima ya baba yangu.

Faraja yangu pekee enzi hizo, ilikuwa kusoma gazeti la Mzalendo, lenye muhtasari wa kesi nzima na kufurahi sana Wakili Lakha alivyokuwa akiwachachafya watu na Mkurugenzi wa mashtaka, wakati huo akiwa William Sekule. Kesi ilikuwa inasikilizwa na Jaji Kiongozi Nassoro Mzava.

Huu ukawa mwanzo wa mimi kuanza kujifunza namna ya kuuliza maswali magumu. Wale viongozi waliokalia kipindi changu cha runinga cha Kiti Moto, wanayajua maswali yangu. Mwalimu wangu wa maswali yale si mwingine bali Murtaza Lakha.

**NAFASI YA MZEE MAYALA**

Kesi hiyo ilihusu oporesheni maalum ya kuwasaka watu wanaofanya mauaji ya vikongwe. Watuhumiwa wawili, Masaga Mabula Mazegenuka wa mjini na Issack Ng'wana Ng'hoboko, walifariki dunia baada ya mahojiano yaliyoendeshwa eneo la Kigoto, nje kidogo ya jiji la Mwanza.

Je, ni kweli Mzee Mayalla alihusika? Je, Wakili Murtaza Lakha, alifanya nini katika kumtetea Mzee Mayalla na kumfanya mtoto wake, Pascal Mayalla atamani kuwa wakili?.

Tukutane Jumapili ijayo katika sehemu ya tatu na ya mwisho ya simulizi ya Safari ya Uwakili ya Wakili Pascal Mayalla.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hivi kulikuwa na ulazima kuvunja majengo haya?



Na Joseph Kulangwa

HAKUNA kiumbe duniani kinachopenda tabia mbaya. Si binadamu si mnyama, wote hupendelea kuona amani na utulivu katika jamii zao vinatamalaki muda wote.

Hiyo ndiyo sababu miongoni mwao wakikosea, hupata adhabu ili kuwarejesha kwenye mstari wa kuwa na tabia njema. Hilo limekuwa likishuhudiwa hata kwa wanyama kushikishana adabu.

Kwa binadamu, tunaelewa na tumekuwa tukishuhudia watu wakiadhibiwa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na viboko, kukemewa, kukaripiwa lakini pia kufanyishwa kazi ngumu.

Lengo la msingi ni kurekebisha na si kuumiza ingawa wakati mwingine adhabu zimekuwa zikitumiwa vibaya kwa kukomoana na hata pengine kusababishiana vilema vya kudumu.

Viboko ni adhabu ambayo imezoeleka sana hususan katika kuwarekebisha watoto, na hiyo imefanya watoto wengi kuogopa kuchapwa na wakubwa zao, iwe nyumbani au hata shuleni.

Nakumbuka adhabu iliyokuwa ikinisikitisha sana utotoni ni ile ya kumnyima mtoto chakula kwa sababu tu amekosa, hivyo kumshindisha au kumlaza njaa. Huko hakukuwa kurekebisha bali kukomoa kama si kutesa.

Hata enzi za utumwa, watumwa walichapwa sana mijeledi pale mabwana walipotaka kuhakikisha wanatii kila walichoambiwa hususan katika kufanya kazi ngumu na za suluba kama za kilimo, kubeba mizigo na zingine.

Wanyama wamekuwa wakiadhibiwa kwa fimbo na binadamu wawapo malishoni, au hata safarini ili mradi binadamu akitaka mnyama afanye anachokitaka yeye.

Hakika mijeledi au viboko vinauma sana mwilini kwani vinajeruhi, mnyama hawezi kulia, wala kujieleza, lakini anapochapwa husikia maumivu makali sana.

Wataalamu wa saikolojia wanasema viboko ni kama mateso kwa binadamu kwa kujirudiarudia, hatimaye humjengea usugu na hivyo kuona tena si adhabu bali mchezo tu wa kawaida.

Ndiyo sababu watoto sugu utawasikia wakisema nitafanya hivi na mama, baba, au mwalimu atanichapa na yatakwisha. Hiyo ni dalili ya usugu, hivyo fimbo hukosa maana ya kuwa nyenzo ya kurekebisha tabia.

Wanadamu tumekuwa tukitesana kwa sababu ambazo wakati mwingine hazina mashiko ila tu kwa kundi moja kudhani watu fulani wamekosea na kisha kuwanyima hata muda wa kujitetea na kujikuta wameangukia kwenye mateso.

Mathalan, hivi karibuni baadhi ya wakazi wa Kizota, Dodoma, walivunjiwa nyumba zao kwa kuwa tu wamevamia eneo la viwanda na kujenga kinyume cha utaratibu.

Kitendo cha kuwavunjia kilichofanywa na uongozi wa Jiji la Dodoma na kuwaacha peupe na mali na familia zao, tena kwenye baridi lililopo, hata kama walikosea kilikuwa ni kinyume cha ubinadamu na kuwasababishia mateso.

Yawezekana ni kweli kuwa Watanzania hao walikosea kuweka makazi ya kudumu eneo hilo, lakini kwa adhabu ya kuwavunjia na kuwafanya washinde na kulala nje kama wanyamapori, si sawa kabisa.

Mbaya zaidi, watu hao wakati wanajenga na kuishi hapo mpaka kuzaliana, wanasema walikuwa wanawaangalia bila kuwahoji au kuwakataza kufanya hivyo, wakati wakiwa katika hatua za awali.

Iweje wasubiriwe mpaka waishi na kujisahau, ndipo wavunjiwe kikatili vile kana kwamba si binadamu? Haipendezi machoni mwa si binadamu wenzao tu lakini hata mwa Muumba wao na wetu pia.

Sawa, hata kama wamepatikana na hatia ya kujenga maeneo yasiyoruhusiwa, kwa nini basi wahusika wasingewaandalia mahali pa kujisitiri na mali zao na kisha wavunjiwe?

Hata kama kuna fidia watapewa, palikuwa na sababu gani ya kuwavunjia hata kabla hawajajua ni wapi wataweka maskani yao ya kudumu na kujenga kwanza ndipo majengo yao ya zamani yavunjwe?

Bila shaka walioshiriki kuvunja kwa matingatinga, walifanya hivyo kwa amri na maagizo ya wakubwa zao na hivyo wasingeweza kukiuka, kwani kukiuka kungewaweka pabaya.

Lakini waliowaagiza, wangefikiria mara mbili kabla ya kuagiza kufanya uharibifu huo wa kimwili na kiakili, na kusababisha usumbufu usio na ulazima kabisa, kwa kuwa nafasi ya kuwaonya kabla hawajaanza kujenga ilikuwapo na hivyo wasingeendelea kujenga.

Inawezekana kabisa mpaka wanajenga eneo hilo, hawakujua kuwa limetengwa kwa ajili ya viwanda, ina maana walioamua sehemu hiyo kuwa ya viwanda, wangeshafika na kuwazuia na wasingeendelea, kwani wanajua wasingeweza kushindana na Serikali.

Hizi ndizo adhabu ambazo binadamu anaweza kusema bora viboko kuliko hii, kwa sababu inawarudisha nyuma kiuchumi lakini pia kuwaathiri kisaikolojia na mwishowe kuichukia Serikali yao, kwa sababu ambazo zingeweza kuzuilika.

**Alamsiki!**

# MIGOGORO YA NDOA CHIMBUKO LA UKATILI

Na Dk. Enock Mlyuka



NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu na kitovu cha familia, jamii, taifa na malezi. Mungu alianzisha ndoa ili watu waingie, waipende na kuifurahia kwa kuwa ndoa ni taasisi ya heri, si ya vita na machinjio ya watu.

Ni mpango asilia wa Mungu kwamba mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu kamili. Amani ni moja ya matunda ya haki na zawadi kutoka kwa Mungu inayomwajibisha binadamu.

Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu na fungani ya binadamu. Kwa mantiki hiyo, amani ni zawadi inayopaswa kutunzwa kwa njia ya kuwa na ndoa imara na malezi yenye dhamira nyofu kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa. Mume na mke katika ndoa ni watu wanaotegemeana ndiyo maana Mungu aliumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane na kutegemeana katika maisha; wafurahi na kufurahishana.

**Migogoro ya Ndoa**

Pamoja na kusudi jema la Mungu la kuanzisha taasisi ya ndoa, wanadamu wameharibu misingi na ladha ya ndoa. Hali hii inapotosha kwa kiasi kikubwa kusudi na maana halisi ya taasisi hii takatifu. Kwa baadhi ya familia, ndoa imegeuka kuwa jela ya nyumbani. Migogoro ya mara kwa mara isiyo na ukomo imekuwa mtindo wa maisha.

Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2022/2023 ya Wizara yake, pamoja na mambo mengine, alibainisha kuwa hadi kufikia Aprili, 2022 wizara ilipokea migogoro ya ndoa 39,571 na kati ya hiyo, 19,262 ilipata suluhu, 15,718 bado iko katika usuluhishi, huku 4576 ikiwa mahakamani. Hii inaonyesha dhahiri kuwa migogoro ya ndoa nchini ni janga la taifa.

**UKATILI KATIKA NDOA**

Kimsingi, migogoro ya ndoa huvuruga ustawi wa familia, hujeruhi nafsi, huondoa hisia za mapenzi na mvuto miongoni mwa wanandoa. Hali kadhalika, huchangia matatizo ya afya kwa sababu ya msongo mkubwa wa mawazo. Migogoro ya ndoa ni chimbuko la ukatili na mauaji katika familia.

**zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo, ni matokeo ya makuzi na malezi wakati wa utoto. Kwa mantiki hiyo, watu wema au wakatili wanatengenezwa katika familia.**

Matukio ya ukatili na mauaji katika familia yanaendelea kutokea katika jamii yetu kutokana na migogoro. Moja ya matukio ya kusikitisha ni tukio la hivi karibuni lililotokea jijini Dar es Salaam ambapo mume alimuua mkewe akiwa kwa wakwe zake. Hali kadhalika huko Buswelu mkoani Mwanza, binti wa miaka 28 aliuawa na mumewe kwa kupigwa risasi kwa madai ya wivu wa mapenzi. Baadaye mumewe naye alidaiwa kujiua kwa kujipiga risasi.

Tukio lingine, huko mkoani Shinyanga, mwanamke anadaiwa kumjeruhi mumewe kwa kumkata uume kwa tuhuma za usaliti wakati Tunduru mkoani Ruvuma, mwanamke alifariki dunia na kuacha mtoto wa miezi 11 kwa kile kinachodaiwa kuwa ameuawa kwa kupigwa risasi kichwani na mchumba wake kutokana na wivu wa mapenzi.

Kama vile haitoshi, Butiama mkoani Mara, mwanamke aldaiwa kumuua mumewe kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali kwa tuhuma za usaliti wakati Serengeti mkoani Mara ilitolewa taarifa na Jeshi la Polisi ya mume kudaiwa kumjeruhi mkewe kwa kumwingizia panga sehemu za siri akimtuhumu kuwa na uhusiano na mwanamume mwingine.

Polisi pia walitoa taarifa kuwa mkoani Ruvuma, mwanamke alimjeruhi mumewe kwa kumkata na wembe sehemu za siri (korodani ya kushoto) akiwa usingizini na kumsababishia maumivu makali. Matukio ya namna hii bado yanaendelea kujitokeza mara kwa mara katika jamii.

Matukio haya yanapotokea katika jamii, hayaathiri wanandoa pekee, bali na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani mfumo wao wa maisha unavurugwa. Wazazi na familia wanazotoka wanandoa huathirika pia kwani hakuna mzazi ambaye angependa kuona mtoto wake anapata matatizo. Taifa nalo linapoteza nguvu kazi muhimu. Hatua za makusudi zinahitajika kuchukuliwa kwa maslahi mapana ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

**Wanandoa wasiishi na vinyongo. Wajenge utamaduni wa kupenda kuzungumza tofauti zao kwa staha, utulivu na uvumilivu kwa kuwa mazungumzo hujenga boma zuri.**

**ROHO YA UKATILI**

Roho ya ukatili hurithishwa kuanzia katika ngazi ya familia kwa sababu tabia na mienendo ya mtu inajengwa katika familia. Wanasaikolojia wanasema zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo, ni matokeo ya makuzi na malezi wakati wa utoto. Kwa mantiki hiyo, watu wema au wakatili wanatengenezwa katika familia.

Kutokana na ukweli huo, familia ni msingi na kitengo kinachomtengeneza mtoto kiroho, kimwili na kitabia (attitudes). Vitengo vingine kama taasisi za dini au shule husaidia tu na kuendeleza msingi uliojengwa katika familia.

Mtoto ambaye hajawahi kushuhudia matendo ya upendo na yenye utu katika makuzi yake, bali migogoro na matendo ya ukatili ya wazazi wake, kuna uwezekano mkubwa wa kuwa mtu katili. Atakapokuwa mtu mzima, kuna uwezekano mkubwa wa kufanya vitendo vya ukatili dhidi ya watu wengine kwa sababu ya vinasaba vya ukatili alivyoambukizwa kutoka kwa wazazi wake kabla au baada ya kuzaliwa.

**NGUVU YA MSAMAHA**

Ndoa ni safari ya maisha ambapo kuna kukosea na kukosana njiani. Kuna umuhimu kwa wanandoa kupata ufahamu wa namna bora ya kukabili migogoro pale inapotokea tofauti miongoni mwao. Ni muhimu wanandoa wawe wepesi kujifunza, kujikosoa, kujisahihisha na kuombana msamaha pale mtu anapohisi kumkosea mwenzake.

Kumjeruhi au kuondoa uhai wa mtu mwingine si suluhu ya tatizo bali ni kinyume cha sheria za haki za binadamu na imani juu ya Mungu Mwenyezi na Maandiko Matakatifu, ambayo wakati wote hutuelekeza itupasavyo kutendeana mema na kuepuka uovu.

Wanandoa wasiishi na vinyongo. Wajenge utamaduni wa kupenda kuzungumza tofauti zao kwa staha, utulivu na uvumilivu kwa kuwa mazungumzo hujenga boma zuri. Mazungumzo yenye staha ni njia nzuri ya kufahamu hisia alizonazo mtu juu ya mwenzake na kutafuta ufumbuzi wa pamoja.

Hakuna ndoa yenye afya njema bila msamaha. Msamaha ni dawa ya furaha ya familia. Msamaha ni muhimu kwa afya ya kihisia na kuendelea kuishi kwa heri. Asiyeomba msamaha na asiyesamehe hana amani katika nafsi yake na hawezi kuwa na ushirika na Mungu.

Watu wasioomba msamaha na wasiosamehe ni wagonjwa wa kimwili, kihisia na kiroho. Siku zote huteseka na kuishi kwa vinyongo na roho ya visasi na maangamizi. Bila msamaha, familia inakuwa uwanja wa migogoro, ngome ya uovu na maafa.

Migogoro ya ndoa ni adui wa maendeleo kwani maendeleo na ustawi wa familia na taifa unategemea ndoa imara. Kwa hiyo, ni muhimu kila mwanandoa ajiheshimu, atambue nafasi, wajibu na mipaka yake katika ndoa ili kuifanya ndoa kuwa baraka.

JUKUMU LA JAMII

Jukumu la kujenga jamii na taifa au kulibomoa, wanalo wazazi, walezi na wanajamii. Wakati umefika sasa jitihada za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia zisiwe za kutoa matamko, kutengeneza mabango, fulana au vipeperushi tu na kutafuta umaarufu. Jitihada hizi lazima ziende sambamba na dhana nzima ya malezi katika ngazi ya familia. Ustawi wa taifa unaanzia nyumbani kwa kuwa uhai wa taifa unategemea uhai wa familia.

Ni wajibu wa wazazi kuwapa watoto malezi bora yatakayowaandaa kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na binadamu wengine. Wazazi wasikwepe wajibu wa kukemea pale inapobidi. Watoto wasioadabishwa na wenye tabia mbaya ni udhia, mzigo, karaha, na fedheha kwa wazazi na jamii. Ukimdekeza mwanao iko siku atakuaibisha na kukusababishia maumivu usiyoyatarajia.

Wahenga wanasema, "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Baba na mama wanapaswa kuishi kwa upendo, amani, utulivu, kuheshimiana na kuwajibika kila mmoja kwa mwenzake ili kurithisha tunu njema kwa watoto na vizazi vitakavyofuata.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JULAI 24, 2022
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 15

**Panga ratiba ya usafi kwenye nyumba yako**



Ukurasa 13

**NJANO MSETO Inavyotoa upekee**




**KATUNIKA**

Ukurasa 16





# KIPINI PUANI

## Urembo wakale usiopitwa wakati

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | A | S | A | L | I |
| ■ | C | ■ | ■ | I | ■ |
| C | H | A | ■ | M | ■ |
| ■ | I | ■ | I | B | A |
| ■ | K | ■ | ■ | U | ■ |
| T | A | N | G | A | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, MWA, SAUMU, LAANA, NYUNGU, LAWAMA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa na babu yake wakitembea kwenda shambani. Babu yake alikuwa akitembea taratibu huku akishikilia fimbo, huku Grace akiwa mbele yake akitembea haraka.

Grace alimuuliza babu yake kwa nini anatembea taratibu na yeye anakwenda haraka?

Babu: Mimi ni mzee nguvu zimeniishia lazima nitembee taratibu na wewe ni mtoto una nguvu za kutembea

Grace: Lakini mwalimu alituambia kuwa taratibu ndio mwendo, kwa hiyo sisi tunaotembea haraka tutapata madhara?

Babu: Mjukuu wangu huo ni msemo tu unamaanisha kufanya kitu kwa taratibu unakuwa makini nacho na utakifanya kwa ubora na sio vingine.

SWALI
Kitunguu maji kina faida gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unamkataa mume wa kwanza, unarudi na talaka mrudiane

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya simulizi ya kijana Pazi na sakata la mkewe aliyemuacha na kuolewa na mwingine, japokuwa na huko hakudumu aliachika.

Kwa wale ambao hawakufuatilia simulizi hiyo, Pazi alikuwa kijana mtulivu mwenye ari na bahati ya kupata kazi. Akampenda binti Halima wakaoana lakini baada ya miezi sita ndoa haikuleta jibu la ujauzito. Ndipo Halima akadai talaka na kuolewa na kijana mwingine aliyempenda awali kijijini kwao.

Yule mume wa pili wa Halima akabahatika kupata naye watoto wawili mapacha. Kijana huyu akaonyesha makucha yake akaanza kumtesa Halima kwa kumpiga, yaani ugomvi kila uchao. Matokeo yake mume huyu wa pili naye akampa Halima talaka.

Hapo ndipo Halima ufahamu ukarudi akaanza kiguu na njia kumsaka mume wa kwanza, Pazi. Lengo likiwa kumshawishi warudiane. Hata hivyo ilikuwa ni vigumu kwani Pazi alikuwa tayari alishaoa mwanamke mwingine Salha na kupata watoto wawili. Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo!

Msomaji wangu, mwendelezo wa pale tulipoishia wiki iliyopita ni kwamba Halima alibahatika kumpata Pazi na kumweleza yote yaliyomkuta kwa mwanaume yule wa pili. Alimkuta akiwa kazini kwake Kunduchi Beach Hotel, hivyo ikabidi amtafutie malazi.

Jambo hilo lilimsumbua sana Pazi na hata aliporejea nyumbani mkewe alihamaki ni kitu gani kilichomkuta mumewe kwa jinsi alivyoonekana mtu wa mawazo.

Asubuhi wakati Pazi anatoka, mkewe akamwita akamuuliza; jana nilikuona hauko sawa na haukunieleza kisa cha wewe kuwa vile. Pazi akajibu kwa kifupi, nikirudi!

Kule hostel ambako Halima alipatiwa malazi, Matroni akamuuliza; Dada wewe unatokea hoteli gani? Akamjibu mimi sifanyi kazi ya hoteli. Mimi nilikuwa mke wa Pazi. Akamuuliza tena; Kwa hiyo umekuja kuchukua matumizi ya mtoto? Hapana, kuna taarifa nimeleta.

Kama alikuwa mkuu mwenzio na kuna taarifa umeleta, kwa nini asikukaribishe nyumbani kwake? Jibu; Ni kweli lakini haiwezekani kutokana na mazingira yalivyo. Matroni akamwandalia chai na baada ya hapo Pazi akapiga simu kuulizia kama mgeni wake ameshapatiwa huduma ya kifungua kinywa.

Kisha Pazi akaagiza atafutiwe bodaboda impeleke kazini kwake ili akamweleze vizuri yaliyompata kimaisha. Halima alipofika akamweleza Pazi mkasa wote hadi kufikia hapo alipo.

Halima machozi yakamtoka na Pazi alipomtizama Halima akajawa na huzuni. Baada ya muda Pazi akamuuliza Halima dhumuni la kumuonyesha talaka. Naye akamweleza ukweli kuwa amekuja kuomba warudiane. Pazi akamjibu, nimeshaoa itakuwa ni vigumu.

Halima hakumwelewa, akasisitiza bila yeye hataweza kuishi kwani uhuni hakuzoea. Pazi akamjibu baada ya kushusha pumzi; Wewe leo ukalale kwa bibi pale Ilala. Nitakupa zawadi kidogo umpelekee bibi na umwambie ni zawadi toka kwa Pazi.

Akamwita mhudumu ampatie Halima chakula, kisha ampeleke kwenye kituo cha mabasi ya Shaffi mjini aweze kuondoka. Pazi akamuaga Halima kwa kumwambia. Tutawasiliana.

Halima alipofika kwa bibi akamueleza yote yaliyotokea. Akampatia na zawadi kutoka kwa Pazi. Bibi alifurahi sana kujua kwamba Halima na Pazi waliweza kuonana.

Pazi kurudi nyumbani toka kazini, mkewe akampokea na alipotulia akamuuliza mbona jana hakuwa na amani? Hapo ndipo Pazi akamweleza yote yaliyotokea bila kificho.

Mpenzi msomaji, simulizi hii inatufundisha mambo kadhaa ambayo yanawakuta wengi.Na somo kubwa lipo kwa upande wa Halima. Kwanza binti huyu aliolewa kwa kutafutiwa mume na wazazi wake.

Pazi baada ya kupata kazi alirudi kijijini wazazi wakamwambia tayari yupo binti wa kuoa. Yeye akakubali ndoa ikafungwa. Akarudi kazini kwake. Ndoa ilipochelewa kujibu mashaka yakamjaa Halima.

Neno la Mungu linasema, “Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua, bali haja ya mtu ikipatikana ni mti wa uzima”. Halima hakuwa mvumilivu ndiyo maana alipoona hashiki ujauzito alilazimisha talaka na kuachana na Pazi.

Upo msemo pia kwamba mvumilivu hula mbivu na pia kawia ufike. Halima pamoja na kuharakisha kuomba talaka, lakini hata kule alikotarajia furaha hakuipata, aliambulia mateso hadi talaka.

Pazi japokuwa alimpenda sana Halima lakini hakuwa na jinsi aliruhusu talaka lakini napo akampata mwenza mwingine aliyempa furaha na amani, pia uzao. Hakika mvumilivu hula mbivu na majuto ni mjukuu!

***Msomaji naishia hapa. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Jamii ichukue hatua kudhibiti ongezeko ubakaji

MATUKIO ya ulawiti na ubakaji wa watoto yanaongezeka kila uchao huku kesi nyingi zikidaiwa kuishia polisi au mtuhumiwa anapopewa dhamana familia zinakaa kuzungumza ili kuyamaliza kifamilia.

Aidha, baadhi ya vijana waendesha bodaboda wanadaiwa kuhusika na matukio hayo hasa wale wanaowabeba wanafunzi kuwapeleka shuleni na kuwarudisha nyumbani kiasi kwamba kuna watoto wamefanyiwa ukatili na kuuzoea au kulazimishwa kuishi maisha ya mateso tangu wakiwa wadogo.

Kwenye shule za msingi na sekondari, matukio hayo yanaongezeka kwa watoto kufanyiwa hivyo na ndugu wa karibu, ambao hulala nao. Mama, baba au mlezi anashtuka, mtoto anakuwa ameshaharibika.

Pia inadaiwa kuwa fedha inatumika kumaliza kesi hizo na wakati mwingine madawati ya jinsia yamelalamikiwa kuwa sehemu ya uharibifu ambao sasa ni maumivu kwa jamii.

Unapokwenda maeneo ya starehe utakutana na vijana wa kiume wa rika mbalimbali wanajiuza, yaani wanaingiliwa kinyume cha maumbile na wanaume wenzao, huku wasichana wakiwa na uhusiano na wasichana au wanawake wenzao.

Vitendo hivi vinaua kizazi kwa kuwa idadi ya wanaume inaendelea kupungua kila siku, huku takwimu zilizopo zikionyesha wanaume ni wachache ikilinganishwa na wanawake. Sasa linapotokea suala la ulawiti, hilo nalo linapunguza idadi yao na kukiweka kizazi hatarini.

Inaelezwa kuwa mwanamume anapofanyiwa kitendo hicho, anatamani kuendelea kufanyiwa ndiyo maana wengi hujiuza ili kupata wa kuwafanyia hivyo. Hili ni kosa kisheria na imekatazwa na kulaaniwa kwenye vitabu vitakatifu vya dini.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ulibaini kuwa baadhi ya watuhumiwa wa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana, wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa mhanga wa vitendo hivyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, hivi karibuni alisema serikali imeanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na inaanza mchakato wa makosa ya ubakaji na ulawiti kuondolewa dhamana.

Katika kuonyesha ukubwa wa tatizo hilo, takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021, zinabainisha kuwa matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa ni 11,499, huku makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa mikoa iliyoongoza kwa matukio ya ukatili na idadi kwenye mabano ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na mkoa wa kipolisi Ilala (489).

Baadhi ya familia zinamaliza kesi hiyo nyumbani. Inapotokea mzazi mmoja anashikilia kuendelea na kesi mahakamani, anaitwa na kukalishwa na ukoo, ikiwamo kutengwa kama atakubali kuendelea na kesi.

Wengi wanaokumbwa na kesi hizi wanatoka familia maskini ambazo wakati mwingine kufuatilia kesi ni usumbufu na gharama. Wakati mwingine wanakutana na usumbufu mkubwa polisi na hospitali na kuamua kubaki nalo moyoni.

Wanaoteseka ni watoto na wazazi wao ambao wametendewa ukatili huo lakini hawana pa kukimbilia kwa kuwa kila eneo hakuna msaada na mwisho matukio kuendelea kutokea.

Mabadiliko ya sheria hiyo kuongeza makali ni hatua nzuri sana kwa kuwa watu wataogopa na kesi zitashughulikiwa inavyotakiwa kwa kuwa ushahidi hautaharibiwa kama inavyofanyika sasa.

Ni muhimu kulinda taifa dhidi ya ongezeko la mashoga ambao wanakuwa hivyo siyo kwa msukumo wa maumbile, bali kwa kufanyiwa ukatili na wachache ambao wananufaika au ni tamaa za mwili.

Lakini ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuchukua hatua mapema taarifa zinapotolewa, kuboresha madawati ya jinsia ili yasiwe kichaka cha rushwa na kuumiza watu, viongozi wa dini walio waadilifu kuendelea kuwahubiri yaliyomema waumini wao na kuwaonya kwa kutumia maandiko matakatifu juu ya vitendo hivyo.

Sheria kufanyiwa mabadiliko ni jambo jema lakini bila kudhibiti rushwa ni sawa na bure kwa kuwa watu wataendelea kufinyanga kesi za namna hiyo ili kupata fedha kwa waliotenda pasipo kuona uharibifu huo ipo siku utabisha hodi kwenye nyumba yake.

Kwa sasa tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, ambayo imeunda kamati mbalimbali kukabili vitendo vya ukatili, lakini ni muhimu kufuatilia hadi ngazi ya chini hasa kwenye shule za msingi na sekondari, lakini pia kuimarisha idara ya ustawi wa jamii, polisi na hospitali ili wafanye kazi kwa hofu ya Mungu na kuogopa kuyaharibu matukio hayo.






Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe juzi alisherehekea siku yake ya kuzaliwa. Katika picha tofauti ni baadhi ya matukio yaliyoambatana na sherehe fupi iliyoandaliwa na The Guardian jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**









# MITINDO

# NJANO MSETO Inavyotoa upekee

RANGI ya njano imekuwa haipendwi sana na baadhi ya watu kutokana na kuwa angavu na yenye kuchagua mavazi.

Watu wanapenda kuvaa nguo zenye rangi hiyo ikiwa na mchanganyiko na rangi zingine kwa imani ya kupendeza zaidi.

Lakini wengi hawajui namna ya kuchanganya rangi ya njano ili kuongeza mvuto kwa watu wanaopenda mitindo.

Unaweza kuvaa nguo ya njano na kisha ukaongeza rangi zingine kwa kutumia mavazi mengine ili kujinogesha zaidi.

Mfano ukivaa shati la rangi ya njano, unaweza kuongeza kwa kuvaa raba nyeusi na suruali ya udhurungi.

Mpangilio huo wa rangi nyeusi, hudhurungi na njano itafanya kazi vizuri katika mwonekano.

Unapochanganya rangi hizi, itafanya kazi vizuri kwa wale walio na ngozi nyeusi na walio maji ya kunde.

Kwa rangi ya njano mchanganyiko unaweza kutengeneza vazi la suti na kuonekana wa kipekee unapotoka matembezini.





URERBO



## UREMBO

Na Mary Geofrey

# KIPINI PUANI

## Urembo wakale usiopitwa wakati





MIAKA ya nyuma ilizoeleka wanawake pekee ndiyo wanastahili kuvaa vipini puani na hata wengine kwa kutoboa kabisa pua.

Katika mitindo ya kizamani, watu walipendelea kuvaa vipini upande mmoja wa pua na mwingine kubakia kawaida.

Urembo huu umeanza muda kidogo na ulivaliwa sana na wanawake wa pwani, siku hizi imekua tofauti kidogo, stahili hii imerudi kwa kasi zaidi na ubora wa hali ya juu.

Sio watu wa pwani tu wanaotumia urembo huu hata wengine pia vile vile sio lazima kutoboa pua na kuvaa upande mmoja wa pua.

Staili imekuja kivingine zaidi waweza vaa katikati ya pua au kutoboa kabisa pua yako na kuweka kipini sehemu zote mbili za pua. Lakini wengi hupendelea moja.

Wasanii wa ndani na nje ya nchi ndiyo wamekuwa wavaaji wakubwa wa vipini hivi kwa namna ambavyo wanataka kuonekana wa tofauti.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# BAGIA ZA DENGU

UNAWEZA kuwa miongoni mwa wale watu ambao walikuwa wanatamani kufahamu jinsi ya kupika bagia za dengu lakini hukuwahi kupata msaada.

Leo tunaelekezana vizuri namna ya kupika bagia za dengu, ili kila mwenye kiu hii kupika nyumbani na kuenjoy na familia yake.

Kwanza kabisa unatakiwa ujue ni chakula kirahisi na hakitumii muda mrefu kuandaa hadi kuiva na kula.

Mahitaji

Unga wa dengu kikombe kimoja, vitunguu maji viwili vilivyokatwa katwa vipande vidogo vidogo.

Vitunguu saumu vilivyo sagwa kijiko cha chai kimoja,

Baking Powder kijiko cha chai kimoja, maji kiasi, chumvi, mafuta ya kukaangia, pilipili na kotmiri ukipenda.

Matayarisho

Kwenye bakuli kubwa changanya unga wa dengu na vitunguu maji, kisha weka vitunguu saumu, kotmiri iliyokatwa katwa na baking powder. Weka chumvi kiasi kidogo.

Weka maji kidogo kidogo hadi mchanganyiko wako uwe mzito kisha uache kwa muda.

Bandika kikaango jikoni na weka mafuta, yakishachemka chota mchanganyiko wako kwa kijiko na kuweka kwenye mafuta. Angalia usiweke mara nyingi sana ili bagia zisijeshikana.

Zikiiva na kuanza kubadilika rangi epua na uweke mahali zitoke mafuta. Hakikisha moto sio mkali sana ili ziive na sio kubabuka.

Andaa tayari kwa kula na kinywaji chochote unachopendelea.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Panga ratiba ya usafi kwenye nyumba yako

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka lakini ninachotaka kueleza ni kwa namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi kama ambavyo ni kinyume kwamba isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo, ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.


Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Na baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Baada ya kusafisha, hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndiyo utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.



## Namna chumba cha chakula kinavyokuwa



UNAPOKUWA na nyumba bora, ni lazima kuwepo na eneo la kulia chakula kukiwa na samani zinazovutia.

Moja ya mambo ya kuzingatia wakati wa kuboresha chumba cha kulia chakula ni kufanya chaguo zuri la viti na meza nzuri ya chakula.

Kutokana na umuhimu wake, zifuatazo ni baadhi ya dondoo ambazo zitakupa mwelekeo kupata seti za samani katika chumba cha chakula.


1: Ikiwa eneo la sebule ni dogo unatakiwa kuweka viti vinne na meza moja ya duara.

2: Kama eneo lako ni kubwa kiasi unaweza kuweka viti vitano na meza ya pembe nne zilizo sawa. Hapa itakuhakikishia nafasi ya kunyanyuka au kuweka kitu kingine.

3.Endapo chumba chako kina ukubwa wa kutosha, unapaswa kuweka viti saba yaani kila upande vitatu na kimoja mbele.

4. Hakikisha watu hawabanani wakati wa kula kwani kwa kufanya hivyo itawapa uhuru.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
DUH!
LEO CHUPA LIME-AMKA NA CHAI MWAMBIE BOSI NIPO MATINGASS!
HUMSHINDI YEYE...
RISEPSHENI
WEWE! USILETE UBABAI, MTEJA SIO MUME MPAKA UMTILIE WIVU
SIO WIVU MFUKUZE HUYO NI BABA WATOTO WANGU ANATAKA NINI HUKU!
'NALIAMSHA' NAFUMANIA
ACHA MKE WANGU JAPO NI DANGA LAKO LAKINI YULE MKEWE MCHEPUKO WANGU
'NAMISHITAKIENI NIMEKONG'OTWA NA MKE WANGU NYIE MWANICHEKA! MWAONA KIOJA?
HATUKUCHEKI ILA WEWE KAMA SISI TUPO SARE SARE HUYU KALA NGUMI, MIMI 'VICHWA!
SIJALI HATA TUKIPINGULIA URAFIKI, KWANZA WEWE MLEVI KAA KWAKO
ENHEEE! HAPO UMENENA, MAANA SENSA HAITATUKUTA VILABUNI.
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KATAWALIWA NA MKEWE, WEWE KIROHO JUU...



Mwanaume wa Kiukraine akiwa analinda mwili wa mtoto wake mwenye umri wa miaka 13, ambaye aliuawa kwa mabomu ya Russia katika mji wa Kharkiv. **PICHA: REUTERS**

# Bandari yalipuliwa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

MLIPUKO mkubwa umesikika katika bandari ya Ukraine siku moja baada ya kufikia mkataba wa kihistoria na Russia ili kuruhusu kurudisha mauzo ya nafaka.

Milipuko kadhaa pia iligonga mji wa Odessa ulioko magharibi mwa Ukraine, mapema jana lakini haijafahamika chanzo cha milipuko hiyo.

Chini ya mkataba uliofikiwa siku ya Ijumaa, Russia ilikubali kutoshambulia bandari wakati wa usafirishaji wa nafaka.

Umoja wa Mataifa ulikuwa umetaja makubaliano hayo ya kuruhusu usafirishaji wa mamilioni ya tani ya nafaka kama msingi wa matumaini.

Oleksiy Honcharenko, mbunge wa eneo hilo, aliandika katika mtandao wa Telegram kwamba milipuko sita ilisikika katika mji huo na bandari yake ilikuwa inawaka moto baada ya shambulio.

Honcharenko aliongeza kuwa vikosi vya ulinzi wa Ukraine vilidungua makombora kadhaa na kwamba ndege za kivita zimekuwa zikiviziana katika anga za mji huo.

**RUSSIA YAONGEZA ORODHA YA MAADUI**

Serikali ya Russia imeongeza orodha ya nchi zisizo rafiki na kujumuisha Ugiriki, Denmark, Slovenia, Croatia na Slovakia.

Waziri Mkuu, Mikhail Mishustin alisema serikali ilipanua orodha ya mataifa ya kigeni yanayochukua hatua zisizo za kirafiki dhidi ya balozi za Russia nje ya nchi.

Nchi hizo zimejumuishwa katika orodha ya kwanza iliyokuwa na nchi za Marekani na Jamhuri ya Czech pekee.Orodha ya pili ina mataifa 48.

Kabla ya vita, Russia ilianza kuzichukulia hatua nchi hizo zisizo na urafiki ikisema kwamba zinafanya vitendo visivyo vya kirafiki dhidi ya yake.

Mnamo Aprili 23, 2021, Rais wa Russia alitia saini amri inayozuia haki ya nchi kama hizo kuajiri raia wake katika balozi zao mjini Moscow.

Mapema mwezi Machi mwaka huu, baada ya kuanza kwa uvamizi wa Russia nchini Ukraine, serikali iliidhinisha orodha nyingine ya nchi na wilaya zisizo za kirafiki.

Kisha orodha ya nchi 48 iliidhinishwa iliyojumuisha mataifa yote ya Umoja wa Ulaya na zingine zikiwemo Australia, Albania, Andorra, Uingereza, Iceland, Canada, Liechtenstein, Mikronesia, Monaco, New Zealand, Norway, Jamhuri ya Korea, San Marino, Macedonia Kaskazini, Singapore, Marekani. , Taiwan (Uchina), Ukraine, Montenegro, Uswisi na Japan.

**VIONGOZI AFRIKA WAKARIBISHA MKATABA**

Viongozi wa Afrika Kusini na Ivory Coast wamekaribisha mkataba uliotiwa saini na Ukraine na Russia kuruhusu usafirishaji wa nafaka kutoka bandari za Ukraine.

Makubaliano hayo yametajwa kuwa makubwa ya kwanza yanayohusisha serikali za nchi hizo mbili tangu kuanza kwa mzozo huo mwezi Februari.

Mkataba huo unalenga kupunguza bei ya juu ya nafaka, na kurejesha usambazaji wa nafaka kwa nchi zinazokabiliwa na uhaba wa chakula.

Akizungumza mjini Pretoria katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na kiongozi mwenzake wa Ivory Coast, Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa, alisema kuzuia nafaka kumewalazimu viongozi wa Afrika kufikiria kwa uzito kuhusu usambazaji wa chakula katika siku zijazo.

"Kuendelea kutegemea kiasi kikubwa cha nafaka kutoka sehemu hiyo ya dunia, kunapaswa kuonekana kama hatari ya kweli kwa watu bilioni 1.3 wa nchi za Afrika" alisema.

Rais Alassane Ouattara, ambaye yuko katika ziara ya kiserikali nchini humo, alisisitiza kuwa Afrika lazima iwe juu ya orodha ya wanaopokea nafaka.

Kiongozi huyo alisema amefurahishwa kuona Rais wa Russia, Vladimir Putin, ameamua kutia saini pendekezo hilo chini ya uangalizi wa Umoja wa Mataifa na Uturuki.

"Pia nilimuomba Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky kulipatia kipaumbele bara la Afrika, kwa sababu ya kudorora kwa uchumi wake na hali ya kijamii katika nchi nyingi," alisema.

**BBC**

## Macron kuanza ziara Afrika

**PARIS,** UFARANSA

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, anatarajiwa kuanza ziara katika mataifa matatu ya Afrika Magharibi.

Ziara hiyo itakayoanza kesho, itakuwa jaribio lake la kujaribu kufufua uhusiano na baadhi ya mataifa ya bara hilo.

Hiyo itakuwa ziara yake ya kwanza nje ya bara la Ulaya tangu kuchaguliwa kwa muhula wa pili, atazitembelea Cameroon, Benin na Guinea-Bissau.

Mada kuu zitakazojadiliwa katika ziara yake ni masuala ya usambazaji wa chakula, kutokana na mataifa ya Afrika kuhofia uhaba wa nafaka uliosababishwa na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Aidha, swala la usalama litakuwa muhimu wakati Ufaransa ikijiandaa kukamilisha zoezi la kuondoka nchini Mali mwishoni mwa mwaka huu.

Ufaransa ina wasiwasi na ushawishi wa mataifa kama Uturuki, China na Russia katika maeneo ambayo inayachukulia kama maeneo yake.

Benin na Cameroon ni koloni za zamani za Ufaransa, lakini Guinea-Bissau ilikuwa koloni la Ureno.

# Sri Lanka yatakiwa kuwalinda wanaokalia majengo ya Ikulu

**COLOMBO,** SRI LANKA

SHIRIKA la kimataifa la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch, limemtaka rais mpya wa Sri Lanka kuviagiza vikosi vya usalama nchini humo, visitishe matumizi ya nguvu yanayokwenda kinyume cha sheria kwa waandamanaji.

Watu wamekuwa wakiandamana kwa miezi kadhaa kuipinga serikali kutokana na mdororo wa uchumi uliosababisha uhaba wa chakula, dawa na mafuta.

Ikiwa ni siku moja baada ya kuapishwa Rais Ranil Wickremesinghe, mamia ya wanajeshi waliokuwa na silaha walivamia kambi ya waandamanaji na kuwashambulia na kuwaondoa ofisi ya rais.

Human Rights Watch ilisema hatua hiyo inatuma ujumbe hatari kwa watu wa Sri Lanka kwamba serikali mpya inakusudia kuongoza kwa kutumia mabavu badala ya utawala wa sheria. Wickremesinghe, ambaye aliwahi kuwa waziri mkuu mara sita, aliapishwa kama rais wiki moja baada ya mtangulizi wake, Gotabaya Rajapaksa, kukimbia nchi baada ya waandamanaji kuvamia makazi yake.

Rajapaksa baadaye alijiuzulu akiwa uhamishoni nchini Singapore

**DW**

MAKALA

# KOZI ZISIZO NA AJIRA VYUO VIKUU ZIFUTWE



Na Magabilo Masambu - 0689157789

JULAI 8, mwaka huu, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) iliwatangazia wananchi na wadau wote wa elimu ya juu nje na ndani ya nchi, kufunguliwa kwa dirisha la maombi ya udahili kwa waombaji wa shahada ya kwanza kwamba limefunguliwa toka siku hiyo hadi Agosti 8 kwa awamu ya kwanza. Hii ilitangazwa baada ya kutangazwa kwa matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka huu.

Sambamba na tangazo hilo, TCU pia ikatoa tangazo lingine kuhusu maonyesho ya 17 ya Vyuo Vikuu yaliyomalizika jana katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Lengo kuu la maonyesho hayo lilikuwa kuwakutanisha wadau wa elimu hasa wanaohitaji kudahiliwa kuonana ana kwa ana na vyuo vya elimu ya juu ili kujifunza mambo mbalimbali kuhusu uchaguzi wa kozi na kadhalika.

Nikiwa mdau wa elimu, nilipata pia nafasi ya kufuatilia kupitia luninga hasa kile kinachoendelea katika maonyesho hayo. Maonyesho haya yamekuwa yanafanyika kila mwaka hasa nyakati za kuelekea kudahiliwa wanafunzi katika vyuo vikuu.

Pamoja na mambo mengine, vyuo vinapata nafasi ya kujinadi kama tunavyofahamu kwamba elimu yetu ni huria kwa hiyo kila mmoja anavutia kwake.

Kutokana na kujinadi huko nikabaini mambo kadhaa. Moja, kutokana na ushauri wanaotoa wenye vyuo husika kwa wanafunzi watarajiwa, lakini wadau wengine pia wa elimu wakiwamo wazazi, nikagundua kwamba kumbe kwenye vyuo vikuu vyetu kuna baadhi ya kozi hazistahili kuwapo, kwa sababu ushauri unaotolewa ni kuhusu tahadhari ya kuchagua kozi za kusoma, kwamba wanafunzi wawe makini wasichaguwe kozi kwa mkumbo.

Ushauri huo ukanifanya nibaki na kigugumizi kwamba ina maana wenye vyuo husika wanazitambua kozi zenye changamoto ya ajira lakini pamoja na ushauri huo wanao utoa bado kozi zile zile zinabaki. Je, kwa wanafunzi ambao hawakupata kufuatilia maonyesho hayo wanajifunza wapi kuhusu kozi zenye ajira ili waziombe? Na kama vyuo husika vinaona kuna tatizo katika kozi hizo, kwa nini wasiwasilishe maombi ya kufutwa kwa kozi hizo TCU?

Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, aliwahi kusema: "Kama unamwona mtu anakuja anafanya mchezo wa kutembea huku amefumba macho na mbele yake kuna shimo refu, wewe uliyefungua macho unaliona shimo lile ukamwacha akatumbukia, akiumia au akifa damu yake itakuwa juu yako."

Damu yake itakuwa juu yako kwa sababu ulikuwa na uwezo wa kumwambia kwamba fungua macho mbele yako kuna shimo. Sasa haitoshi kutoa elimu kwa sababu wanaoipata elimu hiyo ni wachache kati ya wengi wanaoomba vyuo.

Ikiwa watachagua kozi ambazo hazitakuwa na ajira kesho utetezi wake hauwezi kuwa tulitoa elimu kabla ya wao kuomba. Dawa pekee ni kuzifuta kama tunaona hazina tija kwa taifa na kwa mtu mmojammoja. Kama tunaona zina maana basi hakuna haja ya kuwa na elimu ya kutoa juu ya kozi gani waombe. Kuwa na elimu tu kwamba wanaelemishwa namna ya kufanya uchaguzi wa kozi zenye manufaa tayari ni tatizo, kwa sisi watu wa hesabu tunasema kupata kozi nzuri yenye ajira ni "probability"

Najaribu kuona kwamba, kuna umuhimu wa kufanya mapitio ya kozi zote upya tulizonazo katika vyuo vyote vya kati na vya juu. Kwasababu huwezi kuniambia kwamba yuko mwanafunzi anaweza kufahamu kozi gani nzuri wakati hakuwahi kufanya kazi yenye kozi hiyo, yeyote anayejifanya kwamba ana kipaumbele chake lazima ama ameona mahala mtu akifanya kazi hiyo akapendezwa nayo bila kufahamu changamoto zake au ameshauriwa na ndugu wa karibu.

Wako wanaowalaumu baadhi ya wazazi kwamba wanawashauri watoto wao wafanye uchaguzi wa kozi ambazo wakati mwingine si mlengo wa mtoto. Uhakika nilio nao ni kwamba kutokana na mfumo wetu wa elimu na maisha yasiyo na uchaguzi ni vigumu kwa wanafunzi wengi wenyewe kufanya uchaguzi wa kozi nzuri ambao zitawafaa kesho.

Kwa ufupi ni kwamba ni sisi wenye utambuzi kufuta zisizo na tija na kubakiza zenye tija ili kila kozi itakayokuwa inachaguliwa na yeyote imfae. Ikiwa tu mtoto anafika mpaka kidato cha nne hajui kidato cha tano atasoma taasusi(combination) ipi ndiyo iwe chuo kikuu?

Nakubali kwamba wazazi na walimu wanayo nafasi ya kuwashauri kuhusu kozi lakini kama kozi zote zingekuwa za maana wala mambo ya ushauri haya yasingekuwa na maana sana kwakuwa ukirusha shilingi juu "Probability" ya kupata kozi yoyote nzuri inakuwa zaidi ya robo tatu.

Mwisho, unaposema mwache mtoto achague kozi anayoitaka wakati umeweka vigezo vya kuipata kozi hiyo ni sawa na ule msemo wa Nduli Idi Amin Dada kwamba "Unao uhuru wa kusema, lakini siwezi kukuhakikishia baada ya kusema."

Kwa kuwa sasa inaonekana kuna tatizo katika kozi za vyuo vikuu, wazazi, walezi na walimu waendelee kuwashauri vijana kuhusu kozi za kusoma, bado wenye uwezo wa kusema nataka nisome kozi fulani hatujawa nao na hata wakiwepo kuna vigezo vya ufaulu, unaweza kutamani kuwa mwalimu au daktari lakini vigezo huna ukaomba kozi hiyo ukakosa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.coma**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Mwanameka' wimbo uliotumika kwenye 'pepa' kidato cha nne



Na Adam Fungamwango

KATIKA nyimbo zote nchini, ni mmoja tu wa 'Mwanameka' uliopigwa na Dar International, ambao ulitungwa na Marijani Rajab ulichukuliwa na Baraza la Mitihani Tanzania na kuingizwa kwenye moja ya maswali ya mtihani wa Kiswahili ya kidato cha nne mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Pamoja na kwamba nyimbo nyingi za dansi zamani zilitungwa na ustadi wa hali ya juu, baraza lilivutiwa na utaalam wa mtunzi kwenye kuandika kisa kizuri chenye ujumbe murua kwa jamii.

Marijani, ambaye alifariki dunia mwaka 1995, alifanya kazi kubwa sana kwenye utunzi wa wimbo huo, kwani alitumia nahau na misemo, ambayo pia nadhani kwa kiasi kikubwa iliwavutia watunga mitihani na kuuchukua, kuuingiza kwenye mtihani wa kumaliza kidato cha nne mwaka 1991.

Aina hiyo ya utunzi ilisababisha Wizara ya Elimu wakati huo kudiriki kuruhusu wimbo huo kwa watunga mitihani kuuchukua kutunga swali lililokuwa katika kipengele cha ushairi katika mtihani huo.

Ukiachilia mbali kuchukuliwa na Baraza la Mitihani ukatumika kujibu maswali ya mtihani wa Kiswahili lakini pia wimbo huo ulikuwa maarufu mno kipindi hicho.

Nadhani ulikuwa ndiyo wimbo pendwa, uliokuwa ukiimbwa hata barabarani na wanaume, wanawake na hata watoto. Wimbo huo ulisababisha mpaka kuwa na mtindo wa nguo za kike zilizoitwa 'Mwanameka'.

Kinamama na mabinti zao walishona magauni yenye mtindo wa Mwanameka.

Ni wa mapenzi, lakini haukuwa na maneno ya ukakasi. Leo hapa kutakuwa na somo kwa wasanii wa bongo fleva au wanamuziki wa sasa kuwa kutunga nyimbo za mapenzi si lazima utamke maneno ambayo huwezi kuyasikiliza mbele ya watu ambao unawaheshimu.

Na si lazima utaje viungo vya binadamu ili kushibisha wimbo wako uonekane kweli ni wa mapenzi, la hasha. Marijani anatupa somo.

"Kweli penzi, eee, penzi lavunja undugu, watu wakakorofishana, wanakosa kusikilizana, penzi lavunja unyumba ee, nimeyaona kwa Musa, Mwanameka umeleta maneno, umeuvunja unyumba kwa Musa." Unaanza wimbo huo.

Hapo unaweza kuambiwa ufafanue, au ueleze ni kwa nini penzi linaweza kuvunja undugu?

"Mwanameka eee, Mwanameka jirani yangu, mimi naona vibaya, umeponza mama ee, umemponza mwenzio, Mwanameka umeleta maneno umeuvunja unyumba kwa Musa."

Hapa inaanza kuja picha kuwa mwanamama Mwanameka amesababisha Musa kuvunja unyumba wake, kwa nini?

"Uliposikia eee, kwamba Musa ameoa, kaoa mke wa ndoa, Musa kataka kulia, uhuni kaweka kando, ukatumia kila uwezo kuyabadili mawazo ya Musa. Watambua eee, u kipusa mrembo, ukazidisha na mapambo, vipini wanja kwa poda eee, na mwendo wako maringo, Musa macho yake yameona na moyo unaanza sononeka."

Sijui ni kwa nini ila kwa makusudi tu, Mwanameka baada ya kuona jirani yake Musa ameoa, kaamua kumfanyia vitimbi. Hapa Mwanameka anamuwinda Musa kwa udi na uvumba.

"Ukabadili na njia, lazima upite kwa Musa, ukienda sokoni kwa Musa, Musa amevumilia eee, mwisho kapotea njia, kakusimamisha bila kutambua akazungumza neno la mapenzi.

Ulipopata kauli yake ukakubali bila kusita, uliyotaka yamekuwa, kazi ikawa ni moja eee, ni mapenzi motomoto, umempa pendo lenye huba, maneno matamu kama asali."

Aina hii ya maneno ya Marijani, ndiyo yaliyolifanya Baraza la Mitihani kuuchukua wimbo huu.

"Ukichanganya na upendo wako, Musa kanasa kwenye ulimbo, akili zake zimemruka, kwako wala habanduki, kwa mkewe hakumbuki, amekwisha onja asali anataka kuchonga mzinga.

Penzi nalo eee, penzi nalo halina siri na siri si ya watu wawili, mkewe Musa akatambua, naye kadai talaka, hakuliki wala hakulaliki mpaka Musa katoa talaka."

Misemo kama 'kunasa kwenye ulimbo', 'muonja asali huchonga mzinga',' siri si ya watu wawili', wanafunzi wanaweza kuambiwa waeleze maana ya maneno haya na pia kutungia sentensi.

"Baada ya kisa eee, Mwanameka umefanya mkasa, kweli wanisikitisha, mara Musa hutaki wala kumuona hupendi, jama Musa ameumbuka kakosa mwana na maji ya moto."

Hapa pia kuna misemo kama 'baada ya kisa mkasa', na 'kukosa mwana na maji ya moto', ambayo kwa kiasi kikubwa ilichangia wimbo huo kujibia mitihani.

"Kweli Mwanameka umefanya madhambi makubwa. Mambo uliyomfanyia Musa yanasikitisha, hehehe Mwanameka, mkasa uliofanya ni wa mwaka, hehehe bwana Musa, hatokusahau mpaka kufa, tena amekwisha apa mambo ya upuuzi hataki tena, keshaumwa na nyoka akiona unyasi anashtuka, hehehe Mwanameka hebu punguza matata."

Katika wimbo huu, pamoja na kisa cha Mwanameka kuvunja ndoa ya watu, lakini kuna wingi wa nahau, methali na misemo ambayo ndiyo kwa kiasi kikubwa ilitumika kwenye maswali ya mtihani.

Kuna huu wa mwisho 'keshaumwa na nyoka, akiona unyasi anashtuka'. Hebu mimi nisaidie kujibu hapa.

Maana yake ni kwamba mtu akishapatwa na jambo ambalo limemtatiza, kumkwaza, au kumletea matatizo, anakuwa makini sana baada ya hapo.

Historia inasema kuwa Marijani aliyeanza muziki wa ushindani akiwa anasoma Shule ya Sekondari Tambaza, Dar es Salaam, katikati ya miaka ya 1970 alitakiwa kwenda Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) kurekodi nyimbo na bendi ya Safari Trippers na siku hiyo hiyo shuleni kulikuwa na mtihani wa Kiswahili.

Kwa sababu alikuwa akifanya mambo yote mawili kwa wakati mmoja, siku hiyo ilibidi achague moja. Muziki ulikuwa ndani ya damu. Akakacha kwenda shule kufanya mtihani wa Kiswahili na kwenda RTD kurekodi nyimbo na moja ikiwa ni utunzi wake ulioitwa 'Hanifa' ambao ulivuma sana.

Miaka mingi baadaye wimbo wake 'Mwanameka' ukachukuliwa kujibiwa mtihani wa Kiswahili. Huyu ndiye Marijani Rajabu, mwanamuziki ambaye ana historia kubwa kwenye muziki wa Tanzania. Jina maarufu kimuziki aliitwa jabali la Muziki.

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SABRI na Hussein aliwamaliza kwa sekunde chache tu kwa risasi. Nassor na Hassan aliwamaliza kwa kutengeneza ajali iliyotokana na risasi zake mbili kupiga magurudumu ya nyuma ya gari walilokuwa wamepanda. Leo huyu mwanamama, akiwa na binti yake mbona imekuwa ngumu?

Hisia zilizomuingia kichwani mwake zilisababisha mikono yake kufa ganzi, na ikaanza kukosa nguvu. Taratibu akaishusha bastola yake. Akaiweka mfukoni.

Licha ya kwamba hakuna binadamu anayetaka kufa. Jinsi alivyoingia mtu yule mle ndani na kuonyesha sura yenye dalili zote za kuua na ukatili, lakini kitendo cha kurudisha bastola mfukoni kiliwashangaza Hidaya na binti yake Hasnat. Hawakujua aliyetaka kuwatwanga risasi amepatwa na matatizo gani. Waliendelea kuomba Mungu aendelee hivyo hivyo, asiwabadilikie.

Lakini bado walikuwa na hofu, kwani hawakujua hali ile ya kuonekana kughairi ingemchukua muda gani.

Kwa mwendo wa uvivu, akiwa na bastola yake mkononi alilisogelea kochi. Kitendo kile kilisababisha Hidaya na binti yake woga urejee tena upya, kwani hawakumwelewa aliyewavamia nini anataka kufanya.

Akajipweteka kwenye kochi kama mtu aliyechoka kwa kufanya kazi ngumu, huku mama na binti yake wakiendelea kunyoosha mikono juu.

"Shusheni mikono." Aliongea kinyonge. Walitii kwa mshangao.

"We mama njoo ukae hapa kwenye kochi." Akaamuru. "Wewe binti kaa hapo chini."

Baada ya kila mmoja kutii amri, kichwa kilianza kumuuma Prince. Akili ilifanya kazi kwa haraka zaidi kuliko uwezo wake wa kawaida. Kwa mara ya kwanza akili ilimtuma kutotii amri ya baba yake.

"Kama ni kuua nimeshaua watu wanne, lakini huyu mama, au hata binti yake siwezi kufanya hivyo." Alijiambia mwenyewe. Akajiuliza ni kitu gani hasa kimesababisha hivyo?

Kutokana na jinsi alivyolelewa kwa muda mrefu aliishi kiupweke.




**"Najua mnajisikia vibaya, lakini msiwe na wasiwasi. Samahanini sana, sitowafanyia chochote kibaya. Mjisikie huru" Akaongea kama mtu anayeweweseka. Vyote vilivyokuwa vikifanyika, si tu kama viliendelea kuwatisha Hidaya na Hasnat, bali kuwashangaza pia.**

Hakuchanganyikana na watu. Ni kama alikuwa akiishi kwenye gereza la pekee.

Kitu kilichomfanya aishiwe nguvu, ni msisimko wa ajabu uliomkumba ambao hata mwenyewe hakuhisi mara moja umetokana na nini.

Na hii ni baada ya kuiona sura ya binti na Hidaya aliyetumwa kummaliza. Alisoma vitabu mbalimbali vya ubabe, ukatili, kishujaa na historia mbalimbali. Ni vitabu alivyokuwa akivipenda mno. Alisoma pia vitabu vya mapenzi. Hakuvipenda sana kwa sababu alikuwa hajui nini maana yake. Unaanzaje kumpenda mtu? Inakuwaje? Kwa nini inatokea mtu anapenda? Kwa nini kwenye kundi la wanawake, mwanaume, mtu anatokea kumpenda mmoja tu kati ya wote? Hakujua maana yake. Akili ilimtuma kuwa huenda leo amekutana na kitu hicho. "Huku ndiyo kupenda?" Akajiuliza.

Sura na wajihi wa Hasnat ulimvutia. Kwa mara ya kwanza kwenye maisha yake anakutana na kitu kama hicho. Alikuwa hajawahi kumpenda mtu yoyote duniani. Aliyemfahamu ni baba yake tu.

"Najua mnajisikia vibaya, lakini msiwe na wasiwasi. Samahanini sana, sitowafanyia chochote kibaya. Mjisikie huru" Akaongea kama mtu anayeweweseka.

Vyote vilivyokuwa vikifanyika, si tu kama viliendelea kuwatisha Hidaya na Hasnat, bali kuwashangaza pia.

Ni kama vile macho yake yalikuwa yametoka kwenye ukungu mzito. Akaanza kuona ambavyo hakuwahi kuviona huko nyuma. Alipomwambia Hasnat akae chini, tena mbele yake, hakumwambia kwa bahati mbaya.

Alitaka aendelee kuushangaa uzuri wa msichana huyo wa kwanza kabisa kwake kuuona.

Alikuwa ni msichana mbichi kabisa ambaye alikuwa na uzuri wa asili. Labda kutokana na umri wake mdogo alikuwa hajaanza kutumia vipodozi vilivyofurika madukani.

Kila kitu chake kilikuwa cha asili hadi nywele.

Sura yake ilipambwa kwa macho makubwa yaliyolegea kama mtu mwenye usingizi au aliyetoka kulala.

Midomo yake minene kiasi ilizidisha uzuri wa sura yake. Pua ilichongwa vema kabisa na kuzidi kupamba sura yake. Hakuwa mnene wala hakuwa mwembamba sana.

Ambacho alishindwa kung'amua mara moja ni rangi ya ngozi yake kutokana na kwamba ulikuwa ni usiku, lakini anapomtazama hakuwa mweupe sana, wala mweusi tii.

Kwa ufupi kwa muda ule tu aliomuona ingawa ni usiku alijidhihirisha kuwa ni mwanamke mzuri na ametokea kumpenda.

Kitu pekee ambacho alikuwa na uhakika nacho ni kwamba hakuwa na mavazi mazuri ambayo yangemfanya awe kama malaika. Pia hakuwa na matunzo mazuri.

Aliendelea kuushangaa uzuri wa msichana huyo.

"Hivi huyu msichana nikimchukua, akawa wangu, nikamnunulia nguo za gharama, nikampamba akapambika, si atakuwa zaidi ya Cleopatra huyu?" Akawaza. Hasnat alianza kugundua kitu hicho. Kwa sababu aliona tangu mvamizi yule alipoingia robo tatu ya muda wote alikuwa akimtazama yeye tu. Kama msichana yoyote yule, jicho alilokuwa akitazamwa muda wote, na kile kitendo cha kuonekana kuahirisha mpango wake, aliona jamaa inawezekana kuwa 'amekolea.'


"Mwanangu jitulize, wewe ni msichana mzuri sana ujue, basi tu maisha yetu duni, umeshamaliza chuo, najua siku hizi ajira ni ngumu, lakini usijitumbukize kwenye masuala ya ajabu. Hawa vijana hawatokufikisha popote. Tulia, unaweza kupata kazi baadaye. Hakuna anayeweza kukupa kazi wakati ushakuwa mjamzito, ujauzito unatakiwa ukukute tayari una kazi yako na unajitegemea. Ukijituliza unaweza kupata mume wa kukuoa. Hakuna mwanaume atayemuona msichana kirukanjia akamfanya awe mkewe" Hasnat alikumbuka maneno ya mama yake aliyokuwa akimwambia kwa mara, alipomaliza tu chuo.

Na kweli alijituliza, akatulizana mtoto wa watu licha ya kwamba wavulana na kinababa walikuwa wakimuwinda kama simba anavyowinda swala porini, kwa ahadi nono, na hata vitisho pia, lakini wakaambulia patupu.

Leo hii anaona sura ya mtu katili aliyeingia akiwa na nia ya kuua, akighairi ghafla. Na hiyo ni baada ya kuona sura yake. Akaamini maneno ya mama yake kuwa ana uzuri wa asili. Na hata huo alionao ni nusu tu kwa sababu ya uduni wa maisha.

Akashuhudia mbwa mwitu amegeuka na kuwa njiwa. Hakujua cha kufanya. Alichosubiri kusikia nini mvamizi huyo ataongea.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# FURAHIA TANZANIA SEPT 16 UHURU

**Na Saada Akida**

KWAYA ya Moravian Efatha jimbo la Mashariki Ushirika wa Uhuru, wameandaa tamasha la 'Furahia Tanzania', lenye lengo la kuliombea amani taifa, litakalofanyika, Septemba 16, 2022 Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa kwaya hiyo, Jacob Mwashiozya, amesema lengo kuu la tamasha hilo la kusifu na kuabudu ni kumuombea Rais wa nchi Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na kuwaombea amani raia wa nchi hii.

Amesema katika tamasha hilo kutakuwa na kwaya mbalimbali zilizoalikwa ndani na nje ya nchi ikiwemo Joyous Celebration, kutoka Afrika Kusini, inakuja kwa ajili ya kulipamba tamasha hilo.

Amezitaja zingine ni Moravian Efatha kwaya, Uinjilisti kijitonyama, Shangilieni na Edeni zote kutoka Arusha, AIC Chang'ombe, Neema kwaya na Wanasham sham kwaya.

"Waimbaji binafsi watakaohudumu ni pamoja na Paul Obuya kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hapa nchini watakaohudumu ni Neema Simfukwe, Dokta Ipyana na Paul Clement watatumbuiza,". Amesema Mwashiozya.

# Waimbaji Injili waipamba Marekani

MACHO na masikio ya wapenzi wa muziki wa Gospo jana Jumamosi yalikuwa nchini Marekani katika tukio kubwa la burudani ya nyimbo za Injili.

Tamasha hilo linaloitwa 'Imba Together Live Gospel Event' lililowakutanisha waimbaji maarufu kutoka Tanzania, Kenya na Marekani.

Tukio hilo linakuwa sehemu ya kuongeza uelewa wa changamoto mbalimbali zinazowakabili watu ulimwenguni.

Mwaka huu waimbaji kutoka Tanzania waliopamba jukwaa ni Boaz Danken, Dr. Ipyana Kibona, Joel Lwaga, Goodluck Gozbert, Rehema Semfukwe na Grolia Muliro kutoka Kenya.

Waimbaji hao wameungana na waimbaji wenzao kutoka Marekani, Leonard Mbwambo, Edna Matinde, Colin Allured, Kelly Herton, Brett Anderson na Mett Moger.

Aidha mchekeshaji Masanja Mkandamizaji alishiriki kutoa burudani.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SAKA MAMBO SAFI
ARSENAL imempa ofa ya mkataba wa muda mrefu, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20, ambao utamfaya mshahara wake kuongezeka mara mbili, huku pia akiwaniwa na Manchester City. ***(Mail)***

### KOUNDE KUTUA CHELSEA
CHELSEA imeipiku Barcelona kwenye mbio za kuwania saini ya mlinzi wa pembeni wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jules Kounde na watampa mkataba wa miaka mitano mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Telegraph)***

### ANTONY AICHAGUA AJAX
KOCHA wa Ajax, Alfred Schreuder amesema winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22, anapanga kubakia kwenye klabu hiyo licha ya kuwaniwa na Manchester United. ***(ESPN)***

### CHELSEA, SPURS VITANI
CHELSEA na Tottenham Hotspur zinamwania winga wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Newcastle United, Allan Saint-Maximin mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### BELLINGHAM SOKONI
LIVERPOOL wameulizia kuhusu kiungo wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. ***(Fabrizio Romano)***

### DEPAY ANUKIA NEWCASTLE
MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 hatakataa ofa kutoka Newcastle United, imfahamia. ***(Sport)***

### SCAMACCA SAFARI IMEIVA
KLABU ya West Ham inakaribia kumsajili, Gianluca Scamacca mwenye umri wa miaka 23 baada ya kukubaliwa kwa ofa ya ada yao ya pauni milioni 30.5 na Sassuolo kwa mshambuliaji huyo wa Italia. ***(Guardian)***

### KOSTIC ANUKIA ENGLAND
WEST Ham pia inawania kumsajili mlinzi wa kushoto wa Eintracht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Serbia, Filip Kostic mwenye umri wa miaka 29. ***(Fabrizio Romano)***

### WEST YAMFUATA THOMAS
MLINZI wa kushoto wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, Luke Thomas mwenye umri wa miaka 21a anawaniwa na West Ham United. ***(Guardian)***

### ARSENAL YAMKATAA LEMAR
ARSENAL na Everton zimejiondoa kwenye mbio za kuwania saini ya winga wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Thomas Lemar mwenye umri wa miaka 26. ***(L'Equipe, via Express)***

### MAUPAY AWINDWA ITALIA
KLABU ya Brighton imepokea ofa ya pauni milioni 15 kutoka klabu inayoshiriki Ligi ya Serie A, Salernitana ili kumuuza mshambuliaji wake, Neal Maupay mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SADIO MANE AKANUSHA KUTOFAUTIANA NA SALAH

Mshindi huyo wa tuzo ya CAF amesisitiza ana mahusiano mazuri na nyota huyo wa Misri...

**RABAT, Morocco**

SADIO Mane amekataa dhana yoyote ya ushindani na mchezaji mwenzake wa zamani wa Liverpool, Mohamed Salah baada ya nyota huyo mpya aliyesajiliwa na Bayern Munich kushinda tuzo yake ya pili ya Mchezaji Bora wa Afrika wa mwaka katika sherehe zilizofanyika Alhamisi iliyopita.

Mane mwenye umri wa miaka 30, awali alishinda tuzo hiyo mwaka wa 2019, na kuipata tena baada ya kuisaidia Senegal kushinda taji lao la kwanza la Kombe la Mataifa ya Afrika, huku akitangazwa mchezaji bora wa mashindano hayo.

Katika harakati hizo, akawa mfungaji bora wa muda wote wa Senegal, akifunga mabao 33 katika mechi 91 kwa nchi hiyo.

Mane na Salah sasa wamegawanya tuzo nne zilizopita za mwanasoka bora wa mwaka wa Afrika kwa usawa, huku Salah akishinda mwaka 2017 na 2018, na Mane ndiye mshindi wa mwaka 2019 na 2022.

Tuzo hiyo haikutolewa mwaka 2020 na 2021 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Akizungumza na Goal baada ya sherehe hizo, Mane alisisitiza ana uhusiano mkubwa na nyota wa Misri, Salah.

"Watu wakati mwingine husema kuna ushindani kati yangu na (Salah), lakini unajua sijioni kuwa na ushindani na mchezaji yeyote," alisema Mane.

"Tuna uhusiano mzuri, tunatumiana ujumbe kila mara. Nadhani vyombo vya habari kila wakati vinajaribu (kuongeza) mambo. "Unajua sina tu mahusiano na mchezaji mmoja, lakini na kila mchezaji ambaye nimecheza naye duniani.

"Unaweza kumuuliza yeyote unayemtaka katika klabu, au popote nilipopita na niendapo. Nina uhusiano mzuri na wachezaji wote."

Muda wa Mane akiwa na Bayern umeanza vyema, akifunga kwa mkwaju wa penalti dakika tano tu katika mechi yake ya kwanza ya kirafiki dhidi ya D.C. United wiki hii katika ushindi wa mabao 6-2.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
AL AHLY CAIRO
VERSUS
EL GOUNA
1 | 1.29
X | 5.21
2 | 9.21

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ZINCHENKO MALI RASMI YA ARSENAL




**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imethibitisha kumsajili, Oleksandr Zinchenko kwa mkataba wa muda mrefu kutoka Manchester City.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ukraine alikubali maslahi binafsi na Arsenal haraka pamoja na ada ya pauni milioni 30, na nyongeza baada ya pande zote mbili kukubaliana.

Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola alithibitisha kuondoka kwa Zinchenko pale Etihad Jumatano na Arsenal sasa wamehitimisha sakata hilo.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisema: "Tuna furaha sana Alex amejiunga nasi. Ni mchezaji ambaye binafsi namfahamu vizuri na niliendelea kumfuatilia baada ya muda wangu Manchester City.

"Alex ni mchezaji wa ubora wa juu ambaye atatupa chaguzi na uwezo mwingi.

"Sio tu kuhusu nafasi anazoweza kucheza, lakini pia uwezo wa aina mbalimbali ambao atatupa katika safu ya ushambuliaji na ulinzi.

"Alex ni mtu mwenye sifa na tabia nzuri, na nimefurahi kila mmoja amefanya juhudi kubwa kumleta Alex kwenye klabu hii."

# Barcelona yamkera Tuchel

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel amekiri amechoshwa na Barcelona kutaka kumsajili nahodha wa Chelsea, Cesar Azpilicueta na huenda The Blues wakamzuia msimu huu wa joto.

Azpilicueta mwenyewe ameiomba Chelsea kumruhusu aondoke kwa bei ya chini, huku tayari Blues hao wakiwa wameshampoteza Andreas Christensen aliyejiunga na Barcelona.

Lakini Tuchel amesema tathmini tofauti za klabu hizo mbili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 ina maana mkataba wowote uko kwenye hatari ya kuwa wa chini.

"Ni swali gumu kwa sababu sina uhakika kama ninataka kumpa Azpi kile anachotaka. Wakati fulani ni kuhusu kile tunachotaka. Nililinganisha tu ni kiasi gani tulipigania kwa (Kalidou) Koulibaly, napata tabu," alisema Tuchel.

"Koulibaly alikuwa mchezaji muhimu sana kwa Napoli, lakini tunaye mchezaji wa kimataifa wa Hispania ambaye ni nahodha wa Chelsea. Namwona labda yuko kwenye kiwango sawa na (Koulibaly), lakini Barcelona na hawamwoni katika kiwango hicho. Kwa hiyo sina uhakika kama nataka nimpe anachotaka kwani ni mchezaji mkubwa.



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# NABI ATAMANI KULINDA REKODI YA KUTOFUNGWA

**Na Saada Akida**

HUKU nyota wake wakiendelea kuwasili katika kambi ya timu hiyo iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema atakiandaa kikosi chake kivingine kwa kuwapa mbinu mpya ili kuhakikisha rekodi yao ya 'UN BEATEN', wanaiendeleza katika msimu ujao wa 2022/2023.

Akizungumza na gazeti hili, Nabi alisema anaamini silaha kubwa ambayo inapaswa kutumika kwa wachezaji wake ni nidhamu ili kufikia malengo ambayo wanatarajia kufikia kwa msimu mpya.

Nabi alisema msimu huu wanatakiwa kucheza tofauti zaidi ili kufikia malengo kwa kupambana vyema katika kila mechi, wachezaji kuonyesha nidhamu ya hali ya juu pamoja na kujituma.

"Siku zote nimekuwa naamini katika nidhamu kwa wachezaji, kila mmoja akijiheshimu na kuheshimu misingi ya timu, ninaamini tutafanikiwa, wachezaji wakishindwa kujiheshimu na kutambua thamani ya klabu hii, itakua vigumu kwetu kutetea ubingwa na mataji tuliyoyachukua msimu wa 2021/22, silaha ya kwanza kuyalinda mataji yetu ni kila mmoja wetu kuwa na nidhamu," alisema Nabi.

Aliongeza msimu mpya utakuwa mgumu sana kwao kwa sababu timu pinzani zinajiandaa kuvunja mwiko wao ambao wameuonyesha msimu uliopita.

"Jukumu letu sote kulitambua hilo kwa kuhimizana ili kuendelea kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita, kuhakikisha tunaendelea tulipoishia," alisema kocha huyo.

Kabla ya kuanza msimu mpya, Yanga itaikaribisha Simba katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu lakini itatanguliwa na mchezo wa kirafiki wa kimataifa utakaofanyika katika Siku ya Wananchi hapo Agosti 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali, Marco Gaguti akimpongeza nahodha wa timu ya soka ya Wilaya ya Masasi iliyochukua ubingwa wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) katika mkoa huo. **PICHA: BARAKA JAMALI**

# Geita Gold kusajili nane

**Na Shufaa Lyimo**

ILI kukabiliana na ushindani katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA, Geita Gold FC inatarajia kusajili wachezaji wapya nane, imefahamika.

Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Minziro alisema anaamini akipata nyota hao katika nafasi mbalimbali atakuwa na kikosi imara kitakachompa matokeo chanya.

Minziro alisema anaamini ujio mpya wa nyota hao utaimarisha na kikosi chake huku pia akianza maandalizi ya kusaka mechi mbalimbali za kirafiki.

"Ninatarajia kuongeza wachezaji nane kwa ajili ya msimu ujao, ninaendelea kufanya mazungumzo na wachezaji ambao ninawahitaji wajiunge katika timu yetu ili kuunda kikosi chenye ushindani kuelekea msimu ujao," alisema Minziro.

Kocha huyo alisema pia mara baada ya kumaliza mchakato wa usajili, atakiweka hadharani kikosi chake na programu rasmi ya mazoezi itakavyokuwa.

"Wiki ijayo tunatarajia kuanza kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu itakayoanza Agosti 17, mwaka huu, tutajipanga zaidi ili kupata timu imara," Minziro alisema.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 24/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1798 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.69 | 3.39 | 2.41 |
| 14:30 | 2303 | Arminia Bielefeld vs Jahn Regensburg | 1.78 | 3.72 | 4.02 |
| 14:30 | 2365 | Brugge vs Racing Genk | 1.74 | 3.97 | 4.02 |
| 14:30 | 3117 | Hamburger SV vs Hansa | 1.48 | 4.41 | 5.61 |
| 15:00 | 4548 | FK Khimki vs Nizhny Novgorod | 2.23 | 3.19 | 3.14 |
| 15:00 | 4596 | Randers vs Odense | 2.06 | 3.47 | 3.32 |
| 15:00 | 5407 | Aarhus vs Viborg FF | 2.66 | 3.26 | 2.56 |
| 15:15 | 1580 | FC Basel vs Servette Geneva | 1.89 | 3.82 | 3.52 |
| 16:00 | 1466 | IFK Varnamo vs AIK Football | 3.54 | 3.24 | 1.97 |
| 16:00 | 2490 | Helsingborg vs GIF Sundsvall | 1.66 | 3.74 | 4.33 |
| 16:00 | 4545 | Lahti vs Seinajoen JK | 2.70 | 3.24 | 2.37 |
| 16:00 | 5520 | KuPS Kuopio vs Hifk | 1.18 | 5.67 | 12.71 |
| 17:00 | 1142 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.58 | 3.44 | 2.53 |
| 17:00 | 3968 | Aberdeen vs Raith Rovers | 1.66 | 3.63 | 4.51 |
| 17:00 | 4608 | Brondby vs Nordsjalland | 1.88 | 3.66 | 3.71 |
| 17:00 | 5789 | Avai vs Flamengo | 4.11 | 3.53 | 1.74 |
| 17:30 | 1221 | Grasshoppers vs FC Lugano | 2.07 | 3.45 | 3.30 |
| 17:30 | 3835 | Dinamo Moscow vs Torpedo Moscow | 1.57 | 3.89 | 5.39 |
| 17:30 | 4941 | FC Sion vs BSC Young Boys | 4.22 | 4.02 | 1.70 |
| 17:45 | 5295 | Feyenoord vs Lyon | 2.85 | 3.78 | 2.06 |
| 18:00 | 1966 | MSK Zilina vs Dunajska Streda | 2.79 | 3.67 | 2.13 |
| 18:00 | 2436 | Rapid Vienna vs Josko Ried | 1.61 | 3.87 | 4.50 |
| 18:00 | 2515 | TSV Hartberg vs SCR Altach | 2.03 | 3.34 | 3.24 |
| 18:00 | 4744 | Austria Lustenau vs WSG Wattens | 2.27 | 3.30 | 2.80 |
| 18:00 | 5477 | Borac Banja Luka vs FC Sarajevo | 2.28 | 3.15 | 3.05 |
| 18:30 | 3840 | Lokomotiv Plovdiv vs Hebar Pazardzhik | 1.35 | 4.31 | 7.83 |
| 18:30 | 4877 | BK Hacken vs Djurgardens IF | 2.54 | 3.42 | 2.41 |
| 18:30 | 4901 | Kalmar vs Elfsborg | 2.52 | 3.26 | 2.52 |
| 19:00 | 1210 | Valerenga vs Viking | 2.16 | 3.57 | 3.01 |
| 19:00 | 1829 | Sandefjord vs Molde | 4.21 | 4.11 | 1.68 |
| 19:00 | 1964 | Ruzomberok vs Sport Podbrezova | 1.51 | 4.00 | 5.27 |
| 19:00 | 2005 | Haugesund vs Sarpsborg | 2.47 | 3.57 | 2.57 |
| 19:00 | 2110 | Aalborg vs Copenhagen | 3.47 | 3.47 | 2.01 |
| 19:00 | 5507 | Kristiansund vs Odd Ballklubb | 2.40 | 3.55 | 2.65 |
| 19:30 | 2467 | Al Ahly Cairo vs El Gouna | 1.29 | 5.21 | 9.21 |
| 19:30 | 4522 | Ismaily SC vs Pyramids | 4.61 | 3.26 | 1.81 |
| 19:30 | 5313 | Anderlecht vs Oostende | 1.27 | 5.63 | 9.25 |
| 19:55 | 3757 | Cukaricki St vs FK Napredak | 1.52 | 3.83 | 5.50 |
| 20:00 | 3490 | Akhmat Grozny vs Fakel | 1.70 | 3.70 | 4.50 |
| 20:00 | 4140 | Lokomotiv Moscow vs Rostov | 2.32 | 3.30 | 2.90 |
| 21:00 | 1711 | Stromsgodset vs Ham-Kam | 1.85 | 3.67 | 3.82 |
| 21:00 | 4344 | Slavia Sofia vs Levski Sofia | 4.52 | 3.39 | 1.71 |
| 21:15 | 4452 | NK Mura vs Domzale | 1.86 | 3.58 | 3.53 |
| 21:30 | 1232 | Spartak Trnava vs Dukla Banska Bystrica | 1.27 | 4.93 | 9.07 |
| 22:00 | 1152 | Fluminense vs Bragantino SP | 1.90 | 3.23 | 3.77 |
| 22:00 | 1288 | Zamalek vs Smouha Club | 1.67 | 3.77 | 4.73 |
| 22:00 | 1397 | Lokomotiva Zagreb vs NK Osijek | 3.39 | 3.29 | 1.99 |
| 22:00 | 1465 | Palmeiras vs Internacional | 1.49 | 3.87 | 5.88 |
| 22:00 | 3098 | Vojvodina vs Spartak Subotica | 1.47 | 4.02 | 5.88 |
| 22:00 | 3559 | KVC Westerlo vs Cercle Brugge | 2.55 | 3.20 | 2.70 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Julai 24, 2022
Nipashe



Sadio Mane akanusha kutofautiana na Salah

UKURASA 21



Winga wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Kibwana Shomari (kulia), akimtoka mchezaji wa Somalia katika mchezo wa kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Stars ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SOPU AING'ARISHA TAIFA STARS CHAN

## ●●●Ni katika mechi ya kwanza ya safari ya kufuzu CHAN, Manula aumia na...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na mchezaji aliye katika kiwango cha juu kwa sasa, Abdul Suleimani 'Sopu' liliifanya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) kuanza vyema safari ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana.

Ilikuwa ni dakika moja tu baada ya mapumziko, Sopu aliporuka juu kwa kupachika bao kwa kichwa akiunganisha mpira wa krosi uliopigwa na winga, Kibwana Shomari.

Bao hilo lilipatikana baada ya dakika 45 za awali kumalizika bila ya kila upande kushindwa kutikisa nyavu za mwenzake huku kila timu ikicheza kwa mfumo wake, Stars ikicheza kwa kushambulia, lakini Somalia wakizuia zaidi na kushambulia kwa kushtukiza.

Mpira ulianza taratibu, Stars ikipata kona ya mapema lakini haikuwa na madhara na dakika ya kwanza, Somalia walisalimia lango la wapinzani wao kwa shuti la mbali kupitia kwa nyota wake, Anwar Said, lakini mpira huo ulikwenda pembeni.

Kipa wa Stars, Aishi Manula alifanya kazi ya ziada dakika ya 15 kuuzuia mpira mrefu uliopigwa na Anwar usimfikie, Aweys Iman aliyekuwa amewazidi mbio mabeki, lakini kabla hajauweka wavuni, alikuwa ametoka na kuuwahi mpira huo.

Dakika moja baada ya shambulio hilo, Stars ilijibu mapigo kupitia, Feisal Salum 'Feitoto' kama kawaida yake, akiwa nje kidogo ya eneo la hatari aliachia shuti kali ambalo lilipanguliwa na kipa wa Somalia, Said Aweys, mpira huo ukaenda katika miguu ya Sopu, lakini kabla hajauweka wavuni kibendera kikawa juu kuashiria straika huyo mpya wa Azam FC ameotea.

Dakika ya 18, Sopu naye alijaribu bahati yake kwa kupiga shuti la mbali, lililotemwa tena na Aweys, lakini hakukuwa na mtu wa kumalizia, akauwahi tena.

Kibu Denis alikaribia kuandikia Stars bao dakika ya 37, akiwa anatazamana na Aweys, lakini shuti lake lilipaa juu ya lango.

Feitoto alifanya kazi ya ziada kuwatoroka mabeki wa Somalia dakika ya 39 na kuugusa mpira mrefu uliopigwa na Salum Aboubakar 'Sure Boy', mpira ukatoka sentimeta chache ukiwa umempita kipa.

Stars ilianza kipindi cha pili kwa nguvu na kufanikiwa kupata bao dakika moja baada mapumziko lililodumu kwa dakika zote 90.

Manula aliumia baada ya kuokoa shambulio kali la Somalia dakika saba kabla ya mechi hiyo kumalizika, ambapo almanusura isawazishe.

Kabla ya tukio hilo, dakika ya 77, Feitoto aliachia kombora kali lililogonga mwamba wa juu na kurudi uwanjani.

Timu hizo zitarudiana tena Julai 30, mwaka huu kwenye uwanja huo.

## Simba kumenoga, Ouattara afunguka

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Manojkovic akifurahia namna wachezaji wake wanavyoimarika baada ya kupata mechi mbili za kirafiki, beki mpya wa timu hiyo, Mohamed Ouattara amesema sababu kuu iliyomfanya kukubali kutua kwa Wekundu wa Msimbazi ni mipango na malengo endelevu iliyopo klabuni hapo.

Ouattara ambaye ni raia wa Ivory Coast aliliambia gazeti hili anafahamu pia Simba ni klabu kubwa na kongwe ndani ya Tanzania na Afrika.

Beki huyo alisema kabla ya kukubali kutua Simba aliangalia mipango na malengo ya klabu na kuyapenda, vinginevyo asingekubali kusajiliwa na timu hiyo ya Kariakoo jijini Dar es Salaam.

"Nafurahi kuwa hapa sababu ni timu kubwa ndani ya Tanzania na Afrika, ina malengo na mipango mikubwa ambayo kila mchezaji mwenye ndoto angetamani kuwa hapa," alisema Ouattara.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally aliliambia gazeti hili wamefunga usajili kwa upande wa nafasi ya ulinzi na nyota wapya ambao wamebakia na wanatarajia kuwatangaza ni wawili.

"Huo ni ukamilisho wa usajili upande wa mabeki unaotufanya kuwa na mabeki wanne bora kabisa," Ahmed alitamba.

Zoran alisema michezo ya kirafiki ni muhimu kwa kuangalia utimamu wa mwili wa wachezaji wake na jinsi wanavyopokea mafunzo.

Aliongeza anahitaji kila mchezaji kupata nafasi ya kucheza ili kumwona huku akielekeza katika mechi ya kwanza dhidi ya Ismailia, vijana wake kucheza kwa nguvu katika dakika 25 za awali.

"Dakika za mwanzo hakukuwa na tofauti kati ya Ismailia na Simba lakini dakika za mwisho tofauti kubwa ilionekana hasa baada ya wachezaji wangu kuchoka, tunahitaji kuendelea kupata mechi hizi ili kuwaweka sawa," Zoran alieleza.

Jana usiku Simba ilitarajia kucheza mechi ya pili ya kirafiki dhidi ya Al Akhdod inayoshiriki Ligi Daraja la Pili nchini Saudi Arabia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >